



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

**RIPOTI YA JUMLA YA MDHIBITI NA MKAGUZI WA
HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA UFANISI
NA UKAGUZI MAALUM KWA KIPINDI KINACHOISHIA
TAREHE 31 MACHI, 2013**

Machi 2013

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Dira

Kuwa kituo cha ufanisi katika ukaguzi wa hesabu za Serikali na taasisi za umma

Dhamiri

Kutoa huduma ya ukaguzi wa hesabu yenye tija ili kuimarisha uwajibikaji nathamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma. Katika kutoa huduma zenye ubora, ofisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:

Uadilifu

Sisi ni asasi adilifu inayotoa huduma kwa namna isiyo na upendeleo.

Ubora

Sisi ni wanataaluma wanaotoa huduma zenye ubora kwa kuzingatia viwangokubalifu vya ukaguzi

Uaminifu

Tunahakikisha kuwa na kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala washeria.

Mtazamo wa watu

Tunatazamana kukazia zaidi katika matarajio ya wadau wetu kwa kujengautamaduni mzuri wa kuhudumia mteja na kuwa na watumishi wataalamu nawenye motisha wa kazi.

Uvumbuzi

Sisi ni asasi ambayo wakati wote inahamasisha utamaduni wa kupokea na kuendeleza mawazo mapya kutoka ndani na nje ya asasi.

Matumizi bora ya rasilimali

sisi ni asasi inayothamini na kutumia rasilimali za umma ilizokabidhiwa kwaumakini mkubwa.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



Samora Avenue, P.O. Box 9080, Dar es Salaam
Telegram: "Ukaguzi", Telephone: 255(022)2115157/8, Fax: 255(022)2117527,
E-mail: ocag@nao.go.tz, Website: www.nao.go.tz

Kwa kujibu tafadhali nukuu:

Ref. No.FA.27/249/01/2012/2013

28 Machi, 2013

Mheshimiwa Dr. Jakaya M. Kikwete,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P. 9120,
Dar es Salaam.

Yah: Kuwasilisha Ripoti ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi inayojumuisha Taarifa tatu 3) za Ukaguzi wa Ufanisi na mbili (2) za Ukaguzi maalum kwa mwaka wa fedha 2012/2013

Kwa mujibu wa ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iliyorekebishwa 2005) na kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, ninawasilisha kwako ripoti yangu ya nne ya ukaguzi wa ufanisi na ukaguzi maalum zilizofanyika katika mwaka wa fedha wa 2012/2013.

Taarifa hii inajumuisha taarifa tatu (3) za ukaguzi wa ufanisi na mbili za kaguzi maalum katika Serikali kuu na Serikali za Mitaa ambazo zinatarajiwa kuwasilishwa mbele ya Bunge letu Tukufu katika kikao cha Aprili 2013.

Nawasilisha.

Ludovick S. L. Utouh

MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

YALIYOMO

Orodha ya vifupisho	vi
Dibaji	vii
Shukrani	x
Muhtasari	xii

SURA YA KWANZA UTANGULIZI

1.1 Usuli	1
1.2 Mamlaka ya Kukagua	1
1.3 Viwango Vilivyotumika	2
1.4 Lengo la ripoti ya Jumla	2
1.5 Uhakiki wa taarifa katika ripoti hii	2
1.6 Muundo wa Ripoti	2

SURA YA PILI

USIMAMIZI WA UKAGUZI WA MAGARI NA MIPAKA YA KASI

2.1 Tulichokikagua	4
2.2 Umuhimu wake	4
2.3 Tulichokiona	5
2.4 Tulichohitimisha	7
2.5 Tulichopendekeza	8

SURA YA TATU

USIMAMIZI WA MASUALA YA AFYA NA USALAMA MAHALI PA KAZI

3.1 Tulichokikagua	13
3.2 Umuhimu wake	13
3.3 Tulichokiona	14
3.4 Tulichohitimisha	17
3.5 Tulichopendekeza	18

SURA YA NNE

USIMAMIZI WA MIKATABA YA MIRADI YA UJENZI KATIKA HALMASHAURI ZA SERIKALI ZA MITAA

4.1 Tulichokikagua	21
4.2 Umuhimu wake	22

4.3 Tulichokiona	22
4.4 Tulichohitimisha	30
4.5 Tulichopendekeza	31

SURA YA TANO

USIMAMIZI WA UNUNUZI WA VIFAA TEHAMA KATIKA SEKTA YA UMMA

5.1 Tulichokikagua	33
5.2 Umuhimu wake	34
5.3 Tulichokiona	34
5.4 Tulichohitimisha	37
5.5 Tulichopendekeza	39

SURA YA SITA

USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA UVUVI ZIWA VICTORIA

6.1 Tulichokikagua	43
6.2 Umuhimu wake	43
6.3 Tulichokiona	44
6.4 Tulichohitimisha	46
6.5 Tulichopendekeza	47

SURA YA SABA

UDHAIFU ULIOGUNDULIWA WAKATI WA UKAGUZI KATIKA KAZI ZA SERIKALI

7.1 Madhaifu ya jumla yaliyoonekana katika maeneo yaliyokaguliwa	50
7.3 Hitimisho	54
7.3 Mapendekezo kwa Ofisi ya Waziri Mkuu	55

ORODHA YA VIFUPISHO

AFROSAI-E	-	Umoja wa Afrika wa Taasis kuu za Ukaguzi wa nchi zinazozungumza Kiingereza
BMUs	-	Vikundi vya Usimamizi wa Mialo Ziwa Viktoria
LVFO	-	Asasi ya Uvuvi katika Ziwa Viktoria
MCS	-	Vituo vya Usimamizi, Udhibiti na Doria Uvuvi
IUU	-	Uvuvi haramu, usioripotiwa na kudhibitiwa
MLFD	-	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi
ISSAIs	-	Viwango vya Kimataifa vya Taasis Kuu za Ukaguzi wa Taifa
MTEF	-	Muundo wa Matumizi ya Muda Mfupi Serikalini
TANROADS	-	Wakala wa Barabara Tanzania
M&E	-	Ufuatiliaji/Uperembaji na Tathmini
MoLE	-	Wizara ya Kazi na Ajira
TBS	-	Shirika la Viwango Tanzania
TEHAMA	-	Teknolojia, Habari na Mawasiliano
ILO	-	Shirika la Kazi la Kimataifa
SUMATRA	-	Mamlaka ya kudhibiti Usafiri wa Majini na Nchi Kavu
TRA	-	Mamlaka ya Mapato Tanzania
TPF	-	Jeshi la Polisi Tanzania
OHS	-	Usalama na Afya Mahali pa kazi
OSHA	-	Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa kazi
INTOSAI	-	Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi
LGAs	-	Serikali za Mitaa
MDAs	-	Wizara, Idara na Wakala
MoF	-	Wizara ya Fedha
TAMISEMI	-	Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
PPD	-	Idara ya Sera za Manunuzi ya Umma
PPRA	-	Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma
GPSA	-	Wakala wa Serikali wa Huduma ya Manunuzi
PEs	-	Taasis ya Manunuzi/Watumiaji
MCST	-	Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia
TIC	-	Kituo cha Uwekezaji Tanzania
BRELA	-	Wakala wa Usajili na leseni za Biashara
CRB	-	Bodi ya Usajili wa Wakandarasi
NBS	-	Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Dibaji

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti yangu ya nne ya jumla ya ukaguzi wa ufanisi (utendaji) na ukaguzi wa maalum. Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi inahusisha ripoti tatu za ukaguzi uliofanyika kwenye Serikali Kuu (Idara ya Polisi na Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Kazi na Ajira na Wizara ya Fedha). Ripoti ya ukaguzi Maalum, kwa upande mwingine, inahusisha ripoti mbili za ukaguzi uliofanyika kwenye Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Fedha.

Taarifa hii inalenga kutoa kwa wadau wetu (Wabunge, Maafisa wa Serikali Kuu na za Mitaa, vyombo vya habari, wafadhili, asasi zisizo za kiserikali, Asasi za Kiraia n.k) muhtasari wa mambo yaliyoonekana kwenye kaguzi mojawoja tano (5) za ufanisi na Maalum zilizotolewa hadi kufikia mwezi Machi 2013. Maelezo zaidi ya muhtasari huu yanaweza kusomwa kutoka kwenye ripoti kamili zilizotolewa kwa Afisa Masuuli husika.

Taarifa hii inawasilishwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kulingana na Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kifungu cha 34(1) na (2) ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma namba 11 ya mwaka 2008.

Chini ya Ibara 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama inavyorekebishwa, Mdhbiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha kwa Rais kila taarifa aliyotoa kufuatana na Ibara ndogo (2) ya Ibara iliyotajwa. Mara taarifa hiyo inapopokelewa, Rais anamwelekeza mtu husika anayetakiwa kuwasilisha taarifa hiyo mbele ya kikao cha kwanza cha Bunge kabla ya kupita siku saba tokakikao cha kwanza cha Bunge kuanza. Ibara hiyohiyo inamruhusu Mdhbiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha ripoti yake kwa Spika wa Bunge iwapo Rais kwa sababu zozote zile atashindwa kuwasilisha ripoti hiyo kwa Spika kama inavyotakiwa kisheria.

Kutungwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya Mwaka 2008 kumeimarisha uhuru wa utendaji kazi wa ofisi yangu katika kutimiza jukumu lake kikatiba. Haya ni matokeo ya juhudi za Mheshimiwa Rais

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge letu Tukufu. Uhuru wa kufanya kazi katika ofisi yangu utaniwezesha kudhibiti matumizi ya rasilimali za ofisi ikiwa ni pamoja na rasilimali watu na fedha ambavyo vitaniwezesha kufanya kazi yangu bila kuingiliwa na mamlaka yoyote.

Sheria hii imepanua mawanda ya ukaguzi kwa kunipa mamlaka kufanya kaguzi za ufanisi (utendaji), utambuzi, mazingira na ukaguzi maalumu mbali ya ukaguzi wa kawaida wa taarifa za fedha.

Kimsingi, taarifa hii imeniwezesha kutoa maoni huru kwa Bunge kuhusiana na matumizi sahihi na uwajibikaji, uwazi na uadilifu katika matumizi ya rasilimali za umma kwenye maeneo ya usimamizi wa ukaguzi wa magari na mipaka ya kasi barabarani, Usimamizi wa Afya na Usalama mahali pa kazi, Usimamizi wa Mfumo wa bajeti, Usimamizi wa Uvuvi katika Ziwa Viktoria na Usimamizi wa Ununuzi wa vifaa TEHAMA katika sekta ya Umma. Zaidi ya hayo, nia ya ukaguzi ilikuwa kuangalia kama rasilimali zimetumika vizuri ili kuleta matokeo yaliyotarajiwa kwa kuzingatia uwekevu, tija na ufanisi kama ilivyotarajiwa na kupitishwa na Bunge kwenye maeneo yaliyotajwa.

Ni vizuri kufahamu kwamba wakati ofisi yangu inafanya ukaguzi na kutoa taarifa ya utendaji wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Programu na Mashirika ya Umma na shughuli mbalimbali kulingana na sheria na taratibu zilizopo, mwisho kabisa wajibu wa kuhakikisha utekelezaji wa mapendekezo niliyoyatoa upo kwa Maafisa Masuuli.

Ni matarajio ya Bunge kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi watahakikisha kuwa zipo taarifa za fedha kuhusu usimamizi wa rasilimali za umma katika Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya umma kuhusiana na tija na ufanisi kwenye utekelezaji wa programu. Ofisi yangu inachangia kwa kutoa mapendekezo ili kuboresha utendaji katika sekta ya umma. Kwa jinsi hiyo, Serikali kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na ofisi yangu zina mchango mkubwa wa kutoa kwa Bunge katika kujenga imani kwa Umma katika usimamizi wa rasilimali za Umma. Ingawa majukumu yanatofautiana, matarajio ya usimamizi bora ya rasilimali yanafanana.

Ili kukidhi matarajio ya Wabunge na Umma kwa ujumla Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kufanya mapitio ya njia bora zaidi za kufanya ukaguzi na kuongeza wigo wa masuala yanayokaguliwa na hivyo kuimarisha utendaji wa uwajibikaji katika sekta ya Umma. Aidha, tunahakikisha ukaguzi wetu unalenga na kuyapa kipaumbele maeneo muhimu ili kuchangia katika maendeleo ya sekta ya umma. Kwa kuwa kazi ya ukaguzi ni chachu katika usimamizi wa fedha, tunaendelea kujadili masuala yanayoathiri utawala/uongozi katika sekta ya umma, hasa katika utoaji wa taarifa za usimamizi wa fedha na masuala ya utawala bora.

Napenda kutambua mchango wa wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa juhudi kubwa walizofanya katika kutimiza malengo tuliyojipangia licha ya kufanya kazi katika mazingira magumu ambayo ni pamoja na kukosa fedha za kutosha, kukosa vitendea kazi na mishaharaduni na wakati mwingine kufanyakazi kwenye maeneo yasiyopitikakiurahisi.

Natarajia kuwa Bunge litaona taarifa hii kuwa ni muhimu katika kuiwajibisha Serikali kutokana na jukumu lake la usimamizi wa fedha za Umma na utoaji wa huduma kwa Watanzania. Hivyo nitafurahi kupata mapendekezo ya jinsi gani nitaweza kuboresha taarifa yangu hii kwa siku zijazo.

Ludovick S. L. Utouh

MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
S.L.P. 9080,
Dar es Salaam,

28 Machi, 2013

SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioniwezesha kutimiza wajibu wangu wa Kikatiba wa kutoa taarifa hii ya ukaguzi wa ufanisi na upembuzi. Napenda kumshukuru kila mfanyakazi katika ofisi yangu kwa jitihada zao kuniwezesha kutimiza matakwa ya katiba ya kutoa ripoti ya ukaguzi wa thamani ya fedha. Nalazimika kuishukuru familia yangu na za wafanyakazi katika ofisi yangu kwa uvumilivu wao wakati wa uandaaji wa taarifa hii.

Napenda kuishukuru Serikali na Bunge letu Tukufu kwa kuendelea kuisaidia Ofisi yangu katika kutekeleza majukumu yake.

Vile vile, shukrani za pekee ziende kwa wafadhili hasa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden (SNAO), Serikali ya Sweden kupitia Wakala wa Kimataifa wa Maendeleo wa Sweden (SIDA) na Mradi wa Ubora, Banki ya Dunia kupitia mradi wa “the Public Financial Management Reform Programme funding” Serikali ya Ujerumani kupitia GIZ na wote waliotutakia mema ambao walichangia kwa njia moja au nyingine kwa nia ya kuleta mabadiliko katika ofisi yangu. Mchango wao katika kuendeleza uwezo wa wafanyakazi kiakili, kimfumo wa teknolojia ya mawasiliano na nyenzo mbalimbali vimechangia kwa kiasi kikubwa mafanikio yetu.

Hali kadhalika, ninawiwa kuwashukuru wadau wengine wote ikiwa ni pamoja na Afisa Masuuli wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Kazi na Ajira, Wizara ya Fedha, Jeshi la Polisi Tanzania, Wakala wa Afya na Usalama Mahali pa kazi-OSHA na TAMISEMI kwa ushirikiano na kutupatia taarifa muhimu zilizohitajika wakati wa uandaaji wa ripoti mojamoja ambazo ni chanzo cha ripoti hii ya ujumla.

Shukrani za kipekee ziende kwa jamii ya wanataaluma na wataalamu wa kada mbalimbali kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo kikuu cha Mzumbe, wataalamu wa kujitegemea na maafisa wastaafu kwa michango yao ambayo iliboresha ripoti za ukaguzi wa ufanisi kupitia ukosoaji na uhakiki walioufanya wa rasimu ya ripoti.

Napenda kuishukuru Kamati ya Hesabu za serikali (PAC) ambayo itapitia ripoti hii na tunatazamia Maelekezo yake itakayoyatoa.

Pia, ninapenda kuwashukuru maafisa masuuli wote, watumishi wote wa umma Tanzania kote katika Serikali kuu na Serikali za Mitaa bila kuwasahau walipa kodi ambao ripoti hii imewalenga. Michango yao isiyoweza kupimika katika kujenga taifa hatuwezi kukadiria.

Mwisho, napenda kuwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Taifa ya ukaguzi kwa kujituma ili kuwezesha ofisi kufikia malengo yake katika mwaka wa fedha wa 2012/2013. Juhudi zenu zimeinua juu ofisi na nchi yetu. Mwenyezi Mungu awabariki wote kama mnavyojitoa katika kusimamia uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma nchini.

Muhtasari waripoti

Kaguzi za ufanisi ni muhimu kwa sababu zinalenga kuboresha uwajibikajinautendaji waserikalinataasisi zakeili wananchikupokea huduma zenye zinazolingana na thamani ya fedhakutokaserikalini. Kunavigezoambavyo hutumikakatika kuchagua maeneo ya kufanya kaguzi za ufanisi na kaguzi maalumu. Miongoni mwa mengi pamoja nakilio cha ummanaumuhimuwa eneo husika kwa sababuza kijamii na kiuchumi. Sheria yaUkaguzi wa UmmaNamba 11 ya 2008 sehemu ya 28. Inampa mamlaka MdhibitinaMkaguzi Mkuu wa SerikaliyaTanzania kufanya kaguzinaUkaguzi za aina hii katika maeneo husika. Kaguzi hizizilifanyikakulingana na Viwango vyaKimataifavya Taasisi Kuu za Ukaguzi wa Hesabu (ISSAs).

Ripoti hiiya jumlainalenga katika kusaidiaWabunge,Serikali,vyombo vya habari, Umma na wadau wengine katika kufanya maamuzi sahihi ili kutekeleza mapendekezo kwa ajili ya uchumi kuongezeka, tija na ufanisi katika uendeshajiwa shughuli za serikali. Inasisitizwa kwamba ripoti hii ya jumla si mbadala wa taarifa tano zilizoelezewa katika sura tano za ripoti hii. Wizara, Idara na Wakala waliokaguliwa walipewa fursa ya kujadili na kutoa maoni juu ya ripoti ya ukaguzi ya mtu binafsi na kusahihisha makosa

Ripoti hii ya ukaguzi wa ufanisi na ukaguzi maalum una sura saba nazo ni; Utangulizi ambao unatoa taarifa za awali; sura tano zinahusiana na muhtasari wa ripoti mojamoya ikielezea kilichochunguzwa, Umuhimu wake; Tulichogundua, hitimisho na mapendekezo ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi na Afisa Masuhuli. Taarifa hizi moja moja ni usimamizi wa usalama barabarani na ukomo wa mwendokasi Tanzania, Usalama mahali pa kazi mkazo ukiwa katika usajili wa mahali pa kazi na ukaguzi Tanzania; Usimamizi wa mikataba ya miradi ya Maendeleo katika Serikali za Mitaa; Usimamzi wa Manunuzi ya vifaa Serikalini mkazo ukiwa katika vifaa vya TEHAMA na mwisho ni Usimamizi wa shughuli za Uvuvi katika ziwa victoria mkazo ukiwa katika ufuatiliaji/uratibu/usimamizi, udhibiti na doria.

Katika ukaguzi wa usimamizi wa usalama barabarani na mipaka ya kasi, Ukaguzi ulichunguza kama ukaguzi wa magari na mipaka ya kasi

ulilenga vihatarishi na ulisimamiwa ipasavyo kitija na kiufanisi. Ukaguzi uliangalia mipango, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya ukaguzi wa magari na mipaka ya kasi. Jeshi la Polisi(Police Traffic) Makao Makuu naWizara ya Ujenzi kupitia Kurugenzi ya Usalama Barabarani na Mazingira walikuwa wakaguliwa wakuu.

Ukaguzi ulibaini kuwa Ukaguzi wa magari haulengi kwa kutosheleza vihatarishi vikuu, Madereva kurudia makosa Rasilimali za Polisi hazigawanywi kulingana na vihatarishi katika ajali za barabarani, Ufuatiliaji na ufanyajitathmini mdogo na Wizara ya Ujenzi haijaweza kufanya mapitio ya muda baada ya muda katika vikomo kasi nchini takriban kwa kipindi cha miaka 30 iliyopita.

Ukaguzi ulihitimisha kuwa, licha ya idadi kubwa ya mafanikio yaliyosajiliwa na Wizara ya Ujenzi na Jeshi la Polisi, usimamizi wa ukaguzi wa polisi wa magari na mipaka ya kasi katika Tanzania ina udhaifu kadhaa; Kikosi cha Polisi Tanzania kupitia Idara ya Polisi ya Trafiki haina mipango ya kutosha kwa ajili ya ukaguzi uliofanywa polisi wa magari nchini, Ukaguzi wa polisi wa barabarani hausimamiwi ipasavyo na hakuna mfumo wa kuaminika kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini hatua zinazochukuliwa na polisi wa ukaguzi wa magari. Pia ilibainika kuwa adhabu zinazotumika hazisababishi kufikia lengo la kuzuia kurudia kwa makosa. Ugawaji wa rasilimali (kama vile muda, zana za ukaguzi, fedha, magari na rasilimali watu) kwa ajili ya ukaguzi wa magari havikutengwa kwa kuzingatia hatari kama utokeaji wa ajali za barabarani katika mikoa na wilaya mbalimbali.

Katika Ukaguzi wa usimamiziwausalama mahali pa kazi (OHS), ukaguzi ulichunguza kama Kuna usajiliwa usalama-maeneo ya kazi, ukaguzi na rasilimali zilizopo zinasimamiwa kwa tija na ufanisi. Ukaguzi ulijikita katika mipango, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya ukaguzi wa OHS na mgawanyo wa rasilimali. Taarifa zilikusanywa katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia Julai, 2009-Juni, 2012.

Ukaguzi uligundua kuwa OSHA imeweza kusajili asilimia 24 tu ya maeneo ya kazi yanaokadiriwa kuwepo. Hakuna mikakati ya kutambua maeneo ya kazi ambayo hayajasajiliwa nchini. Hakuna rejista ambayo inaonyesha maeneo ya kazi ya muda au yaliyofungwa. Ukaguzi ulibaini adhabu kwa meneo ya kazi yasiyosajiliwa

hazitekelezwi ipasavyo. Ukaguzi maeneo ya kazi hayapangwi kulingana na vihatarishi. Maeneo ya kazi ambayo ukaguzi wake unaonekana kuwa wa gharama kubwa haupewi kipaumbele ikilinganishwa na mapato yanayotarajiwa kukusanywa. Hakuna tathmini iliyofanyika kutathmini ubora wa ukaguzi uliofanyika dhidi ya viwangovilivyowekwa. Ilibanikwa kuwa kuna Udhaifu katika kufuatilia ukaguzi na hatua dhaifu zilichukuliwa. Uchunguzi wa afya kwa wafanyakazi haufanwyi vya kutosha Kamati ya OHS haina ufanisi. Hakuna mkakati wa kutosha kwa ajili ya kukadilia mapato yatakayo kusanywa pamoja na mapato halisi. Ukosefu wa mfumo sahihi kwa kuhakiki mtaji wa uwekezaji kama ilivyo ripoti wa na wateja. Wizara mama, Wizara ya Kazi na Ajira haijatoa kianzio cha kutosha kwa OSHA ili kuwawezesha kufanyakazi yake kama vile utambuzi na usajili wa maeneo ya kazi, ukaguzi wa maeneo ya kazi, kufanya ukaguzi waafyanausalama, ufuatiliaji na tathmini ya maeneo ya afya na usalama kazini. Wizara ya Kazi na Ajira (MoLE) haijafanya M&E juu ya shughuli za OHS zinazofanywa na OSHA na pia haijatengeneza viashiria vya utendaji kwa ajili ya shughuli za OHS nchini.

Tulihitimisha kuwa asiliamia 24 tu za maeneo ya kazi yamesajiliwa. OSHA haina mipango maalum kwa ajili ya kutambua maeneo ambayo hayajasajiliwa na kusajili maeneo yaliyokwisha tambuliwa. Ukaguzi haupangwi na kutekelezwa vya kutosha, kamati za OHS na wawakilishi wake hawatumiwi ipasavyo. Vilevile, mafunzo hayapangwi na kutekelezwa sawasawa. Wizara ya Kazi na Ajira haijafanya ufuatiliaji na tathmini vya kutosha

Katika usimamizi wa miradi ya maendeleo katika Serikali za Mitaa, ukaguzi ulichunguza kama serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Sekretarieti za Mikoa ina mfumo madhubuti kwa ajili ya kusimamia mikataba ya miradi ya ujenzi wa maendeleo katika Halmashauri kwa ajili ya kupunguza ucheleweshaji, ongezeko la gharama na kasoro ubora katika miradi ya maendeleo iliyokamilika. Lengo lilikuwa hasa kuangalia mipango na bajeti kwa ajili ya miradi ya ujenzi, utekelezaji wa miradi na Ufuatiliaji, tathmini na utendaji na utoaji taarifa ya miradi ya ujenzi. Ukaguzi ulilenga Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGAs).

Tuligundua kuwa: makadirio ya muda na gharama kwa ajili ya kukamilisha miradi ya maendeleo hayana uhalisia. Makadirio yaliyotolewa na Serikali za Mitaa yalikuwa yamepangwa kukamilika katika muda wa awali kuliko ukweli halisi. Hii ni pamoja na gharama kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ukosefu wa utaratibu wa kuhakikisha ubora katika hatua ya awali ya mipango; utekelezaji wa miradi usio wa wakati; uhaba wa fedha wa miradi ya ujenzi na ukosefu wa ufuatiliaji wa mipango na ukaguzi juu ya utekelezaji wa mradi.

Tulihitimisha kuwa Serikali za Mitaa hawakupanga vya kutosha na kubajeti miradi ya maendeleo. Ucheleweshaji, kuongezeka kwa gharama na masuala ya ubora havikushughulikiwa vya kutosha na Serikali za Mitaa na mamlaka nyingine husika.

Katika ukaguzi wa usimamizi wa manunuzi ya vifaa katika sekta ya Umma hasa katika manunuzi ya vifaa vya TEHAMA, lengo lilikuwa kutathmini kiwango ambacho mamlaka husika zimefanya ufuatiliaji na tathmini juu ya manunuzi ya umma na iwapo hatua sahihi zimechukuliwa ili kuboresha namna ambavyo mfumo wa manunuzi unafanya kazi.

Mkaguliwa mkuu katika ukaguzi huu ni Wizara ya Fedha hasa kupitia Idara ya Sera za Manunuzi ya Umma(PPD). Ukaguzi ulilenga serikali kuu na hasa Wizara 4 (nne). Taarifa zilizopatikana kutoka Wizara nne zilizochaguliwa zimetumika kuonyesha udhaifu katika utekelezaji wa mfumo uliopo wa ufuatiliaji. Wizara hizo ni: Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Wizara ya Mambo ya Ndani; Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; na Wizara ya Viwanda na Biashara. Wengine ni Wakala wa Serikali wa huduma ya Manunuzi GPSA na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Ukaguzi umegundua kuwa, Hakuna Ukadiriaji wa Mahitaji unaofanywa na wizara mbalimbali matokeo yake vifaa vinavyonunuliwa havitumiwi ipasavyo. Wizara ya Sayansi na Mawasiliano haijaandaa miongozo na vigezo vya vifaa vya TEHAMA na kuiratibu. Wanunuzi (Procurement Entity) hazifuati kiwango cha ukomo kilichowekwa na GPSA; Wanunuzi-PE hawafanyi ukaguzi wa kutosha wa vifa vya TEHAMA

wakati vinapowasilishwa; Wanunuzi hawafuatilii vya kutosha utendaji wao wenyewe na utendaji wa wagavi. Divisheni ya Sera ya Mipango ya Manunuzi imeshindwa kuandaa Sera ya Manunuzi ya Taifa na Viwango vya manunuzi kwa vyombo vya serikali ingawa kiasi cha fedha kilichotolewa kilikwisha tumiwa. Pia divisheni ya sera na mipango ya manunuzi haijawahi kufuatilia na kutathmini mfumo wa manunuzi katika wizara, Idara na wakala wa serikali (MDAs).

Ukaguzi ulihitimisha kuwa wanunuzi PE hawajandaa sawasawa mahitaji na vigezo; Kuna tofauti katika gharama na ubora wa vifaa vya TEHAMA kati ya wanunuzi (PE). Hakuna ufuatiliaji wa kutosha wa wagavi licha ya kuwa ni moja ya majukumu yao. Divisheni ya Sera ya Manunuzi ya Taifa haijaipa kipaumbele ufuatiliaji na kutathmini utendaji wa manunuzi katika miaka mitatau iliyopita.

Katika ukaguzi wa Usimamizi wa shughuli za Uvuvi katika ziwa Victoria, ukaguzi ulichunguza kama Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi (MLFD) imeratibu, dhibiti uvuvi haramu na kufanya doria kwa ufanisi na tija ili kukabiliana na tatizo la uvuviwasangara uliopita viwango (Overfishing)katikaZiwa Victoria.Ukaguzi ulitumia taarifa za kipindi cha miaka mitatu kuanzia Juni 2008 hadi Desemba2011. Pia taarifa zilikusanywa kutoka wilaya 15 zenye shughuli za uvuvi katika mikoa ya Mwanza, Kagera na Mara. Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi (MLFD) ina wajibuwa kuandaa, kutekeleza, kupelemba (ufuatiliaji) na kupitia marekebishoya muundo wa serana kanuni za uvuvi Tanzania. Pia, Ofisiya Waziri Mkuu -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) hutekeleza sera hizo kupitia halmashauri husika.

Ukaguzi uligundua kuwa, Kiasi cha samaki kinachokadiriwa kubaki ziwani kipo chini kupita kiasi kilichopendekezwa. Asilimia 50 ya wavuvi na vyombo vya uvuvi katika Ziwa Victoria havikusajiliwa Ufuatiliji wa karibu wa shughuli za uvuvi ziwani hautoshi, Vikundi vya usimamizi wa mialo BMUs vina uwezo mdogo katika kuzuia uvuvi haramu, usioripotiwa na kudhibitiwa. Taarifa za Uvuvi hazisimamiwi vya kutosha. Wizara hajaweka kiasi cha juu kwa ajili ya uvuvi wa Sangara kwa mwaka hii ni ktokana na aina ya uvuvi wenyewe. Hatua duni zimechukuliwa kukabiliana nauvuvi haramu, usioripotiwa na kudhibitiwa. Taarifa za uvuvi haramu, usioripotiwa na kudhibitiwa

hazijasimamiwa ipasavyo katika ngazi mbalimbali na Kampeni za uelimishaji hazijafanyika kwa kiasi cha kutosha.

Ukaguzi ulihitimisha kuwa hatua za udhibiti hazikutekelezwa vya kutosha. Jukumu la Ufuatiliaji/uratibu halikutekelezwa vya kutosha ili kupunguza kupungua kwa Sangara na hatua duni zimechukuliwa kupambana na uvuvi haramu, kutoripotiwa kwa taarifa za uvuvi na kutodhibitiwa.

Madhaifu ya jumla katika shughuli za serikali yaliyogunduliwa katika ukaguzi wa ufanisi ni Upungufu katika usimamizi wa kaguzi mbalimbali, Ufuatiliaji na tathmini hafifu, Mipango hafifu, Mgawanyo mdogo wa rasilimali, Uratibu usioridhisha kati ya wadau husika; Utekelezaji wa sheria husika usioridhisha na wmfumo dhaifu wa usimamizi wa taarifa mbalimbali (“data”).

Kwa ujumla kaguzi zinahitisha kuwa, baadhi ya malengo yaliyopangwa na serikali yanaweza kuwa vigumu kufikiwa kutokana na madhaifu mengi yaliyobainishwa Madhaifu hayo ni katikamipango ya shughuli mbalimbali za serikali, kufanya kaguzi katika sekta husika, mgawanyo wa rasilimali, uratibu wa wadau muhimu katika sekta husika, utekelezaji wa adhabu mbalimbali na mfumo wa usimamizi wa data katika vyombo mbalimbali serikali huathiri kufikiwa kwa malengo ya kiuchumi, tija na kiufanisi (Economy, Efficiency and Effectiveness) katika programu, shughuli na miradi ya serikali.

Tulipendekeza yafuatayo kwa Ofisi ya Waziri Mkuu

Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe kwamba vyombo vya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa vinafanya yafuatayo:

Usimamizi wa Kaguzi: Kaguzi za shughuli mbalimbali za Serikali inapangwa ipasavyo; kaguzi zinaelekezwa kwa namna ambayo zitatatua matatizo katika maeneo hatarishi katika sekta husika; Kaguzi zisimamiwe ipasavyo; Kuwe na miongozo rasmi kwa ajili ya kufanya kaguzi mbalimbali; Kuweka kumbukumbu za kutosha za Matokeo ya kaguzi na Kuna ufanisi katika ufuatiliaji wa matokeo ya kaguzi.

Ufuatiliaji na Tathmini: Inafuatilia na kutathmini utendaji wa vyombo vyote vya serikali Tanzania; Vyombo vyote vya Serikali vinaandaa mipango ya ufuatiliaji na kutathmini M&E na kuitekeleza ipasavyo na kuhakikisha taarifa za utendaji zinaandaliwa kwa vipindi; Vyombo vyote vya serikali vinaandaa viashiria muhimu vya utendaji na kuvipima ili kutathmini utendaji wao na Kutengeneza/kuandaa utaratibu Taifa wa kina wa ufuatiliaji na kutathmini shughuli/programu katika ngazi ya Taifa.

Mipango ya Shughuli za Serikali: Kufanya tathmini ya mahitaji kikamilifu Taasisi na vyombo vyote vya serikali kuandaa mipango ya kuendesha shughuli zao na mipango ya maendeleo. Pia kuwe na mawasiliano ya kutosha na ya wakati kati ya vyombo husika

Mgawanyo wa Rasilimali: Kuwe na mfumo wa wazi wa kupata rasilimali na mgawanyo katika sekta na shughuli mbalimbali za serikali.

Uratibu kati ya Wadau Muhimu: Uratibu wa kifanisi kati ya taasisi/vyombo vya serikali na wadau mbalimbali wenye wajibu wa kutoa taarifa au huduma muhimu Tanzania.

Utekelezaji wa sheria: Hatua sahihi za kisheria zinachukulia kwa taasisi za kiserikali/waharifu ili kuepuka hasara au utendaji mbovu.

Mfumo wa Usimamizi wa data

Kuna uratibu wahifadhidata muhimu, wa kina na wa kuaminika kwa ajili ya kupata taarifa kutoka katika taasisi mbalimbali za serikali.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli

Kaguzi za ufanisi ni muhimu kwa sababu zinalenga kuboresha uwajibikaji na utendaji wa taasisi serikali ili wananchi wapate huduma zinazolingana na thamani ya fedha Kuna vigezo ambavyo hutumika katika kuchagua maeneo ya kufanya kaguzi za ufanisi na kaguzi maalumu. Miongoni mwa mengi ni pamoja na kilio cha umma na umuhimu wa eneo husika kwa sababu za kijamii na kiuchumi.

1.2 Mamlaka ya kukagua

Ukaguzi wa Ufanisi awali ulilenga kuhimiza utumiaji wa rasilimali wa kitija na kifanisi katika sekta za serikali. Kuwapatia Bunge, Wizara, Idara, Wakala na Serikali za Mitaa msingi katika maamuzi ya kiseru ili kuborasha Ufanisi. Pia Kuwapatia taarifa za kuwaweza kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa mapendekezo mbalimbali na kuwatia moyo sekta za umma katika kuanzia utaratibu kutoa taarifa za utendaji ili kuchangia uwajibikaji zaidi.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Tanzania ana mamlaka ya kisheria ya kufanya ukaguzi wa Ufanisi kupitia Sheria ya Ukaguzi Na. 11 ya mwaka 2008. Kifungu cha 28 cha Sheria hii kinasema “Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa lengo la kuthibitisha uwekevu, tija na ufanisi katika matumizi ya fedha au rasilimali za taasisi za umma, anaweza kukagua, kuchunguza na kutoa ripoti, kadiri atakavyoona inafaa, juu ya:

- (a) *Matumizi ya fedha na rasilimali za umma katika wizara, idara, mamlaka za mitaa na mamlaka nyingine za serikali;*
- (b) *Utekelezaji wa majukumu ya maafisa masuuli, wakuu wa idara na wakuu wa taasisi mbalimbali za umma;*

1.3 Viwango vya Ukaguzi

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ni mwanachama wa “International Organization of Supreme Audit Institutions (INTOSAI)” and Umoja wa Afrika wa Ofisi za kuu za Ukaguzi wa nchi zinazozungumza Kiingereza (AFROSAI-E). Kuwa mwanachama wa taasisi/jumuiya hizi za Kimataifa, NAO inapaswa kufuata matakwa yote ya Viwango vya Kimataifa vya ukaguzi “International Standards of Supreme Audit Institutions (ISSAIs) inavyotolewa na INTOSAI”.

Ukaguzi ulifanyika kwa kufuata viwango vya kimataifa vya “International Standards of Supreme Audit Institutions (ISSAIs)”. Viwango hivyo vinataka timu inayofanya ukaguzi kupanga na kufanya ukaguzi ili kupata vidhibiti sahihi na vya kutosha ili kutoa matokeo ya ukaguzi na kuhitimisha kwa misingi ya jinsi lengo la ukaguzi lilivyo na kuleta matokeo yanayoboresha baada ya kutekelezwa. Katika muhtsari wa kaguzi zote za ufanisi na maalum katika ripoti hii ya jumla, timu ya ukaguzi imehakikisha ina vidhibiti muhimu na kutoa matokeo ya ukaguzi kwa kufuata malengo ya ukaguzi.

1.4 Lengo la Ripoti hii ya Jumla

Ripoti hii ya jumla inalenga kuwapa taarifa muhimu Waheshimiwa Wabunge, vyombo vya habari, umma pamoja na wadau wengine kufanya maamuzi yatakayoongeza uwekevu, tija na ufanisi katika shughuli za serikali.

Ripoti hii haikusudii kuwa mbadala wa ripoti tano ambazo zimeelezwa kwa muhtasari katika sura zinazofuata. Ili kuweza kupata uelewa zaidi juu ya matokeo ya ukaguzi kwa ajili ya kuwahoji maafisa masuuli katika maeneo husika, msomaji anashauriwa kusoma ripoti kamili.

1.5 Uhakikishaji wa taarifa mbalimbali zilizotumika katika ripoti za ukaguzi wa ufanisi

Wizara, Idara na Wakala waliokaguliwa walipewa nafasi ili kuweza kujadili na kutoa maoni yao katika kaguzi moja moja na kurekebisha makosa.

1.6 Muundo wa Ripoti

Sehemu zilizobaki za ripoti hii zinahusisha muhtasari wa ripoti tano kwa minajiri ya kuelezea tulichokagua, Umuhimu wake, tulichokiona, tulichohitimisha na tulichopendekeza.

Sura ya pili inatoa muhtasari wa masuala muhimu kuhusiana na ukaguzi wa ufanisi wa Usimamizi wa Magari na Mipaka ya kasi.

Sura ya Tatu inatoa muhtasari wa masuala muhimu kuhusiana na ukaguzi wa ufanisi wa Usimamizi wa Afya na Usalama mahali pa kazi hasa ikilenga katika usajili na ukaguzi wa mahali pa kazi Tanzania.

Sura ya Nne inatoa muhtasari wa masuala muhimu kuhusiana na ukaguzi wa ufanisi wa Usimamizi wa Mfumo wa Bajeti Tanzania hasa ikilenga katika uandaaji wa bajeti, Mipango, Ufuatiliaji na tathmini.

Sura ya Tano inatoa muhtasari wa masuala muhimu kuhusiana na ukaguzi wa ufanisi wa Usimamizi wa Ununuzi wa Vifaa vya TEHAMA katika sekta ya Umma.

Sura ya Sita inatoa muhtasari wa masuala muhimu kuhusiana na ukaguzi wa ufanisi wa Usimamizi wa Uvuvi katika Ziwa Viktoria.

Sura ya Saba inatoa muhtasari wa udhaifu wa jumla uliogunduliwa wakati wa ukaguzi wa shughuli za serikali.

SURA YA PILI

USIMAMIZI WA UKAGUZI WA MAGARI NA MIPAKA YA KASI

2.1 Tulichokichunguza

Ukaguzi ulichunguza kama ukaguzi wa magari na mipaka ya kasi ulilenga vihatarishi na ulisimamiwa ipasavyo kitija na kiufanisi. Ukaguzi uliangalia mipango, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya ukaguzi wa magari na mipaka ya kasi. Matokeo ya ukaguzi yalilenga kupata majibu ya maswali makuu mawili. Maswali yaliyotumika katika ukaguzi huu ni kama yalivyoelezwa hapa chini:

Swali la ukaguzi 1: *Je, usimamizi wa huduma ya ukaguzi unalenga vihatarishi na unaendeshwa kitija na kiufanisi?*

Swali la ukaguzi 2: *Je, mipaka ya kasi imewekwa kwa kuzingatia maeneo hatarnishi na kusimamiwa kitija?*

Jeshi la Polisi (Polisi Trafiki Makao Makuu) na Wizara ya Ujenzi kupitia Kurugenzi ya Usalama Barabarani na Mazingira walikuwa ndio wakaguliwa wakuu. Ukaguzi pia uliwahusisha wahusika wengine muhimu katika Usimamizi wa Usalama Barabarani na Mazingira ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya kudhibiti Usafiri wa Majini na Nchi Kavu 'SUMATRA' na Wakala wa Barabara Tanzania 'TANROADS'.

Ukaguzi ulilenga kipindi cha miaka minne kuanzia Januari, 2007 - Desemba, 2010. Takwimu zilikusanywa kutoka mikoa tisa (9) kati ya 21 ya Tanzania Bara. Barabara sita (6), za Mkoa na Wilaya zilihusishwa wakati wa ukaguzi huu ikiwa ni pamoja na 'abiria na magari ya bidhaa.

2.2 Umuhimu wake

Ajali barabarani ni moja ya suala kubwa katika jamii na afya ya jamii nchini Tanzania. Hali ya usalama barabarani imekuwa ikizorota. Serikali ya Tanzania imeanzisha mipango mbalimbali katika kujaribu kupunguza tatizo la ajali barabarani. Baadhi ya mipango ni pamoja na kuanzishwa

kwa leseni mpya ya kuendeshea gari kwa nia ya kudhibiti ongezeko la idadi ya madereva wasiokidhi viwango au wale walio na leseni bandia. Mpango mwingine ulikuwa ni kuanzishwa kwa vidhibiti mwendo kwa lengo la kupunguza kasi ya baadhi ya magari ya biashara.

Katika kipindi kati ya mwaka 2000 na 2008, jumla ya idadi ya ajali barabarani iliongezeka kwa asilimia 42 (kutoka takriban 14,500 kwa 20,600). Idadi ya majeruhi imepanda kwa asilimia 27 na idadi ya watu waliofariki iliongezeka kwa asilimia 67. Hii ni mara 30 hadi 40 juu zaidi kuliko nchi za Ulaya Magharibi. Mbali na kupoteza maisha ya wengi, athari za ajali za barabarani imeathiri kwa kiasi kikubwa sana uchumi wa nchi.

Kulingana na takwimu za polisi wa magari, sababu za kibinadamu imechangia asilimia 75 ya ajali za barabarani mwaka 2008, wakati sababu nyingine kama vile Mitambo na hali ya barabara imechangia asilimia 25 iliyobaki.

katika mwaka 2009, Serikali ya Tanzania ilitengeneza Sera ya usalama ya taifa kwa mujibu wa mkakati wa 'E' tano ili kupunguza / kuzuia ajali. Pamoja na juhudi hizi, hali ya ajali za barabarani nchini Tanzania bado ni mbaya.

2.3 Tulichokiona

2.3.1 Ukaguzi wa magari haulengi kwa kutosheleza vihatarishi vikuu

Ukaguzi ulibainisha kuwa ukaguzi wa magari haukuweka kipaumbele kushughulikia mambo makubwa ambayo yanachangia ajali za barabarani. Kipaumbele kiliwekwa katika vigezo kama vile mambo ya mitambo yenye hatari ya asilimia 12 katika ajali za barabarani na sababu nyingine kama vile leseni ya kuendesha gari barabarani, ukosefu wa pembetatu na kifaa cha kuzimia moto n.k. ambavyo huchangia kidogo sana katika ajali za barabarani. Sababu za kibinadamu zimechangia hadi asilimia 74 ya ajali zote zilizotokea barabarani nchini Tanzania katika mwaka 2010.

2.3.2 Madereva kurudia makosa

Malengo ya kuweka adhabu hayakuweza kufikiwa kwani madereva

wengi waliendelea kurudia kutenda makosa yaleyale waliyokwisha tenda na kupewa adhabu. Zaidi ya theluthi mbili ya madereva kati ya 445 waliitikia katika dodoso yetu kwamba waliendelea kurudia makosa yaleyale kwa zaidi ya mara tatu katika mwaka mmoja. Sababu zilizotolewa na polisi wa magari kuhusiana na madereva kurudia makosa ni ukosefu wa kumbukumbu ambazo zingetumika kufuatilia wavunja sheria za barabarani ambayo inaleta ugumu kutoa adhabu tofauti na iliyotolewa mwanzo.

2.3.3 Rasilimali za Polisi hazigawanywi kulingana na vihatarishi katika ajali za barabarani

Mgawanyo wa rasilimali watu (maafisa wa polisi wa magari) na vifaa vya ukaguzi kama vile bunduki, vipimia kasi ya mwendo na pombe (kichambuzi upumuaji) kwa ajili ya ukaguzi wa magari na madereva katika mikoa haukufanyika kwa kuzingatia vihatarishi katika ajali za barabarani.

Mikoa ambayo ina hatari kubwa (idadi ya ajali mbaya / km) imetengewa maafisa polisi wa barabarani wachache ikilinganishwa na mikoa mingine ambayo ina hatari kidogo kiasi katika ajali za barabarani. Vile vile, mikoa yenye idadi kubwa ya ajali ilikuwa kichambuzi pumzi ‘breath analyzers’ 1-2 tu na vipimia mwendo kasi vichache.

2.3.4 Ufuatiliaji na ufanyajitathmini mdogo

Ufuatiliaji wa ukaguzi wa polisi wa trafiki katika Jeshi la Polisi ni mdogo. Kati ya vigezo vinne ambavyo Jeshi la Polisi linatumia kufuatilia utendaji wa wafanyakazi wake kuhusiana na ukaguzi wa magari, vigezo vitatu vifuatavyo ni mara chache vimekuwa vikifuatiliwa: ni kwa kiwango gani madereva wamekaguliwa, upatikanaji wa vifaa vya ukaguzi, na tathimini ya utendaji wa wafanyakazi wa Kikosi cha Polisi Tanzania.

Kigezo cha nne, kama mapato yaliyokusanywa kutokana na faini kutoka kwa madereva wanaovunja sheria za barabarani zimefuatiliwa ipasavyo na taarifa ya mara kwa mara inawasilishwa Ofisi ya Jeshi la Polisi Mkoa kutoka kwa ofisi ya polisi ya wilaya. Ukaguzi unaofanywa na polisi wa barabarani haujafanyiwa tathmini kuangalia kama matakwa ya ukaguzi

na malengo yanafikiwa.

Wizara ya Ujenzi haijaweza kufanya mapitio ya muda baada ya muda katika vikomo kasi nchini takriban kwa kipindi cha miaka 30 iliyopita. Hii imesababisha kutoelewa ufanyajikazi wa vikomo kasi. Vile vile, hakuna uchambuzi uliofanyika kutokana na ajali za barabarani ili kufanya mapitio katika vikomo kasi vilivyopo au kuweka vipya.

2.4 Tulichohitimisha

Pamoja na idadi kubwa ya mafanikio yaliyosajiliwa na Wizara ya Ujenzi na Jeshi la Polisi, usimamizi wa ukaguzi wa polisi wa magari na mipaka ya kasi katika Tanzania ina udhaifu kadhaa.

Kikosi cha Polisi Tanzania kupitia Idara ya Polisi ya Trafiki haina mipango ya kutosha kwa ajili ya ukaguzi uliofanyika polisi wa magari nchini. Udhaifu huu umesababisha ukaguzi wa polisi wa magari kutopewa kipaumbele; kushindwa kushughulikia mambo muhimu ya hatari (kama vile mambo ya kibinadamu) na ukaguzi umelenga mambo ambayo huchangia kiasi kidogo katika ajali za barabara.

Ukaguzi wa polisi wa barabarani hausimamiwi ipasavyo na hakuna mfumo wa kuaminika kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini hatua zinazochukuliwa na polisi wa ukaguzi wa magari.

Pia ilibainika kuwa adhabu zinazotumika hazisababishi kufikia lengo la kuzuia kurudia kwa makosa. Ugawaji wa rasilimali (kama vile muda, zana za ukaguzi, fedha, magari na rasilimali watu) kwa ajili ya ukaguzi wa magari havikutengwa kwa kuzingatia hatari kama utokeaji wa ajali za barabarani katika mikoa na wilaya mbalimbali.

Wizara ya Ujenzi haijafanya juhudi kubadilisha kikomo kasi kulingana na mabadiliko ya hali ya barabara. Mipaka ya kasi ya sasa iliwekwa 1973 wakati hali ya barabara nchini ilikuwa tofauti kabisa na hii ya leo. Vile vile, mfumo wa sasa wa kufuatilia hali ya ajali za barabarani ni dhaifu. Hakuna uratibu wa hifadhidata ambayo ni muhimu kwa ajili ya mapitio ya mipaka ya kasi.

2.5 Tulichopendekeza

2.5.1 Mipango ya ukaguzi wa trafiki

Jeshi la Polisi Tanzania linatakiwa kuhakikisha kuwa inapanga ipasavyo ukaguzi wake. Hii inaweza kufanyika kwa kuhakikisha kwamba:

1. Uwekwaji wa polisi wa trafiki unazingatia takwimu za uchambuzi wa ajali za barabarani na unalenga barabara na maeneo ambayo ajali za barabarani zinatokea mara kwa mara, na pia tabia ya madereva wenye uendeshaji usiosalama na wavunja sheria za barabarani.
2. Mafunzo kwa polisi wa trafiki lazima yapanuliwe na kuboreshwa ili kupata polisi wataalamu wenye ujuzi katika kutumia vifaa vya kisasa, mbinu na mikakati, na kuwa na uwezo wa kufanya kampeni ya utekelezaji wa sheria ya barabarani kama ilivyopangwa kiufanisi.
3. Viashiria vyenye tija vitumike kufuatilia utendaji, ikiwa ni pamoja na idadi ya kutumia na mashtaka iliyotokana na matumizi ya vifaa vya kisasa kaka vile kifaa cha kupima pombe na rada ya mwendo kasi.

Jeshi la Polisi Tanzania linapaswa kuandaa mpango utakaoorodhesha vihatarishi katika utekelezaji wa sheria ya Usalama Barabarani, hatua za kuchukua kukabiliana na vihatarishi hivyo na gharama inayotarajiwa, na pia kutoa ratiba kwa ajili ya kutathmini na kurekebisha jitihada za mawasiliano.

Jeshi la Polisi Tanzania lazima, ndani ya maeneo linalowajibika, liandae mpango wa utekelezaji ili kutambua na kushughulikia vihatarishi vikubwa katika usalama barabarani vinavyotokana na madereva. Mpango huo ushughulikie:

1. Upangaji wa maafisa wa polisi wa trafiki uwe na uwezo rahisi wa kuwabadilisha nchini kote katika maeneo yatakayotambuliwa kuwa na hatari kubwa kwa usalama

- barabarani;
2. Maeneo ya vituo vya ukaguzi ‘check points’ kwa kuangalia/kukagua tabia za madereva lazima yalenge mitandao ya barabara kimkakati (iko kwenye maeneo yenye hatari kubwa katika usalama wa barabarani); na
 3. Kufanya ukaguzi wa kuhama hama ‘mobile inspection’ katika njia muhimu.

2.5.2 Usimamizi wa ukaguzi wa trafiki

Jeshi la Polisi Tanzania linapaswa kuhakikisha kwamba:

1. Miongozo juu ya kufanya udhibiti wa trafiki kwa kutumia vihatarishi / ukaguzi unatengenezwa na kutumika na maafisa polisi wote wa trafiki.
2. Ukaguzi trafiki unazingatia vipaumbele kulingana na hatari maalum kama vile kasi na ulevi;
3. Taarifa ya ajali za barabarani zinakusanywa kiusahihi na kikamilifu ili kuruhusu mapitio ya uchambuzi na uhandisi kufanyika zaidi ya mashtaka ya kisheria; na
4. Inaweka jinsi ya kupata taarifa zote ikiwa ni pamoja na historia ya kumbukumbu ya wavunja sheria za barabarani na sahihi kusimamia usalama barabarani katika njia jumuishi. Hii itasaidia Jeshi la Polisi kuweka na kufuatilia maelezo ya usalama kwa madereva mbalimbali na kutathmini kiwango cha hatari husika.

2.5.3 Mgao wa rasilimali za ukaguzi wa trafiki

Jeshi la Polisi Tanzania linapaswa kuhakikisha kwamba:

1. Rasilimali muhimu (rasilimali watu, fedha, ukaguzi zana na magari) zimetengwa vya kutosha na maeneo yote na hatari kubwa ya ajali za barabarani yanapewa kipaumbele cha juu;
2. linaweka mpango wa rasilimali watu katika Usalama

Barabarani/polisi wa kuangalia utekelezaji wa sheria barabarani haraka iwezekanavyo. Mpango huu lazima ulingane na mpango mkakati, na utaje idadi inayotakiwa ya maafisa wa polisi wa trafiki na wakaguzi na uhodari wao, na iweke pamoja mkakati wa kuajiri ili kukidhi mahitaji hayo;

3. Linatengeneza mkakati wa mafunzo ambayo yanaendana na mpango wa rasilimali kwa ajili ya Usalama Barabarani / polisi wa kuangalia utekelezaji wa sheria barabarani. Mkakati ulenge kushughulikia matakwa ya uhodari, mahitaji ya mafunzo, kozi ili kukidhi mahitaji hayo, na ratiba kwa mafunzo ya kawaida; na
4. Vituo vya trafiki vya kudhibiti ufuataji wa sheria za barabarani vinawekwa kwenye maeneo yanayotarajiwa kuwa na athari kubwa ili kupunguza idadi ya ajali zinazotokea barabarani.

2.5.4 Ufuatiliaji na tathmini ya ukaguzi wa trafiki

Ili kuboresha ufuatiliaji tathmini na ukaguzi wa Polisi wa trafiki nchini, Jeshi la Polisi Tanzania linatakiwa:

1. Kuhakikisha kwamba linafuatilia na kutathmini mara kwa mara matokeo ya hatua mbalimbali walizochukua. Wanapaswa pia kufanya uchambuzi / utafiti zaidi kushughulikia suala la trafiki kama moja ya sababu hatarishi katika ajali za barabarani;
2. Inatengeneza seti ya viashiria vikuu vya upimaji wa namba na maelezo katika muda mfupi na muda wa kati kutathmini kiwango ambacho usalama wa barabara/ utekelezaji mipango ya trafiki na mipango hatua zinazochangia kufikia malengo yake ya muda mrefu ya kupunguza idadi ya ajali za barabarani / shambulio; na
3. Linaweka programu ya viashiria hatari vya taifa kwa aji-

li ya utekelezaji wa sheria za Usalama Barabarani haraka iwezekanavyo, ili kuwa na njia sanifu ya kutathmini hatari kwa mgawanyo wa rasilimali chache. Polisi wa Trafiki lazima aweke katika kumbukumbu maamuzi yote yaliyotolewa katika mchakato wa kuchambua vihatarishi.

2.5.5 Adhabu kwa wavunja sheria barabarani

Jeshi la Polisi Tanzania linapaswa kuhakikisha kwamba matumizi ya adhabu kwa wavunja sheria wa barabarani inatumika ipasavyo na ni kwa mujibu wa sheria na kanuni kama zilivyoainishwa; na waje na njia ya kutathmini ufanisi wa adhabu zinazotolewa.

Kumbukumbu ya mfumo wa hifadhidata (database) ambapo historia ya wavunja sheria za barabarani unawekwa, hivyo kuwafanya wavunja sheria za barabarani kuwa makini kutorudia makosa yaleyale.

Uwekaji wa mipaka ya kasi

Wizara ya Ujenzi ihakikishe kwamba mipaka ya kasi katika barabara mbalimbali inawekwa vizuri. Hii inaweza kufanyika kwa kuhakikisha kwamba:

1. Kasi sahihi kwa kila aina ya barabara katika mtandao inaamuliwa;
2. Kunawekwa vikomo kasi ambavyo ni vya kuaminika kulingana na aina ya barabara, hali na mazingira yake; na
3. Kunawekwa mipaka ya kasi kwa msingi wa kufikia kiwango cha chini ukilinganisha na wastani wa hatari ya utokeaji wa ajali.

2.5.6 Usimamizi wa mipaka/vikomo kasi

Wizara ya Ujenzi ihakikishe kwamba mipaka ya kasi katika barabara mbalimbali inasimamiwa vizuri. Hii inaweza kufanyika kwa kuhakikisha kwamba:

1. Vikomo kasi vinafanyiwa mapitio upya mara kwa mara

kulingana na matumizi ya ardhi na hali ya barabara (kubadilika kwa kikomo kasi kutegemee kama kuna maboresho au uchakavu katika hali ya barabara);

2. Vikomo kasi vilivyopo vifanyiwe mapitio kila baada ya mara kwa mara ili kuona kama vinaendana na kasi sahihi kulingana na barabara inavyofanya kazi;
3. Uwekaji wa kikomo kasi utanguliwe na uchambuzi wa kina wa matumizi ya ardhi na aina ya ajali za barabara zilizotokea na aina ya barabara;
4. Kuna ufuatiliaji wa hali ya barabara wa mara kwa mara na ajali za barabarani zitokeazo katika barabara zetu, na
5. Mfumo wa kulazimisha ufuataji wa kikomo kasi unatekelezwa unaanzishwa kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kama kamera ya kupimia kasi.

SURA YA TATU

USIMAMIZI WA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI

3.1 Tulichokichunguza

Serikali ya Tanzania ilianzisha Wakala ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), chini ya Wizara ya Kazi na Ajira na kuwapa wajibu wa kuhakikisha usalama na afya katika maeneo yote ya kazi, kwa kuweka na kutekeleza sheria na viwango ambavyo vitazingatiwa na waajiri katika kila sehemu za kazi. OSHA ilianzishwa kupitia Sheria ya Wakala, Na. 30 ya 1997 chini ya Programu ya marekebisho ya Umma ya Agosti 1, 2001.

Kwa majibu wa sheria ya Usalama na Afya Kazini Namba 5 ya 2003, OSHA inahusika na ubainishaji, usajili, ukaguzi, usimamizi na tathmini ya masuala yote ya Usalama na Afya Kazini Tanzania Bara na inatoa mafunzo, elimu na msaada kwa waajiri na wajiriwa katika maeneo ya kazi za yaliyosajiliwa. Sheria AUK inashughulikia masuala ya waajiri na wajiriwa kupitia OSHA.

Dhumuni la ukaguzi ilikuwa kuchunguza kama usajili maeneo ya kazi, ukaguzi na rasilimali zilizopo zimesimamiwa kwa ufanisi na unaendesha kwa tija. Ukaguzi unahusisha mipango, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya ukaguzi wa usalama na afya kazini na magawanyo wa rasilimali.

Mawanda ya ukaguzi yanahusisha kipindi cha miaka mitatu kuanzia Juni, 2009 - Juni, 2012. Takwimu zilikusanywa kutoka mikoa minne (4) kati ya mikoa 24 ya Tanzania Bara. Mikoa minne iliyotembelewa ilichaguliwa kutoka katika kanda nne. (yaani mkoa mmoja kila kanda). Wastani wa maeneo 6-10 ya kazi yalitembelewa katika kila mkoa kwa mikoa minne iliyotembelewa wakati wa ukaguzi.

3.2 Umuhimu wake

Asilimia ya waajiriwa wote katika dunia wanaofikiwa na huduma ya afya kazini inakadiriwa kutoka asilimia 10 hadi 20. Mwaka 2003 na 2004, taarifa ya idadi ya ajali Tanzania Bara ilikuwa 1,692 na 1,889 kwa mtiririko huo na kiasi jumla ya shilingi 668,500,000 zilitumika kwa ajili

ya kufidia waathirika wa ajali hizi.

Kulingana na Shirika la Kazi Duniani (ILO) ripoti ya 2011, inakadiriwa kuwa watu milioni 2.34 walikufa kutokana na ajali inayohusiana na ajali au magonjwa sehemu za kazi katika mwaka 2008, ambayo vifo milioni 2.02 vilisababishwa na aina mbalimbali za magonjwa na vifo 321,000 vilihusiana na ajali kazini. Hii ni sawa na wastani wa zaidi ya vifo 6,300 vinavyohusiana na kazi kila siku.

Pamoja na juhudi hizi, usalama na afya kazini katika Tanzania bado ni tatizo kubwa na waajiriwa katika sekta zote za kijamii na kiuchumi kila siku wanaathirika.

Kulingana na taarifa za utangulizi hapo juu katika, Mdhimiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliamua kufanya ukaguzi wa ufanisi juu ya usimamizi wa usalama na afya kazini.

3.3 Tulichokiona

3.3.1 Hali ya usajili wa maeneo ya kazi

OSHA imeweza kusajili maeneo ya kazi 6,599 kati ya maeneo yanayokadiriwa kufika 27,500 katika Tanzania ambayo ni sawa na asilimia 24 ya maeneo yote ya kazi. Hakuna mikakati ya kubainisha maeneo ya kazi mabaya hayajasajiliwa nchini. Hakuna mpango maalumu uliondaliwa na ofisi za OSHA za kanda zinazoonyesha wakati na jinsi Mamlaka itakavyobaini maeneo ya kazi yasiyosajiliwa ndani ya mamlaka zao. Maeneo ya kazi ambayo yapo pembezoni mwa mji, maeneo ya vijijini na mikoa mingine ambayo ipo mbali na ofisi za kanda za OSHA wanakabiliwa na hatari ya uwezekano wa kutosajiliwa kabisa na OSHA. Hakuna rejista ambayo inaonyesha maeneo ya kazi ya yaliyopo katika muda fulani au yaliyofungwa. Maeneo ya kazi mengi yalianzisha shughuli zao kwa kipindi kabla ya kuandikishwa na hawakuadhibiwa.

3.3.2 Upangaji wa Ukaguzi wa usalama na afya mahala pa kazi

Ubora wa mipango ya ukaguzi ni duni. Mipango ya ukaguzi iliyopitiwa haikuwa na vipengele muhimu vya mipango mizuri kama vile malengo mahususi kwa ajili ya ukaguzi, kiasi cha mafanikio, mgao wa rasilimali katika suala la nani anawajibika kwa lipi wakati wa ukaguzi na aina gani ya zana ukaguzi wa au vifaa vinavyohitajika kama vile taarifa za

ufuatiliaji na tathmini za ukaguzi zilizopangwa.

Maeneo ya kazi ambayo yapo katika maeneo ya mbali hayakukaguliwa ipasavyo. Hii ni kwa sababu moja ya masuala muhimu yanayozingatwa wakati kupanga ukaguzi ni gharama itakayotumika kukagua dhidi ya mapato yanayotarajiwa kukusanywa kutoka katika ukaguzi uliofanyika.

Ukaguzi maeneo ya kazi haupangwi kulingana na viashiria vya hatari. Hakuna tathmini ya hatari iliyofanyika na OSHA kubaini maeneo ya kazi yenye magonjwa na ajali nyingi kazini. Hakuna kumbukumbu ya kimaandishi ya tathmini ya hatari toka kwa waajiri na kujumuishwa kwa pamoja na OSHA ambayo inaweza kutumika kama msingi wa kupanga ukaguzi. Hivyo, ukaguzi hauna kipaumbele cha kuzingatia maeneo ya kazi ambayo ni duni zaidi na yanakubikwa vihatarishi vya matukio ya ajali kazini na magonjwa.

3.3.3 Ukaguzi wa usalama na afya unaofanyika mahali pa kazi

Maeneo ya kazi ambayo ukaguzi umeonekana kuwa ni wa gharama kubwa ikilinganishwa na mapato yanayotarajiwa kukusanywa kutokana ukauguzi huo yamekuwa yakipewa kipaumbele cha chini bila kujali ni kwa jinsi gani uendeshaji wao wa kazi ni hatarishi.

Vile vile, ilionekana kwamba fomu ya ukaguzi inayotumika sasa haina maelezo ya kina jinsi gani ukaguzi ufanyike. Hii ni kwa sababu fomu imebuniwa kwa kutumika wakati wa kupanga ukaguzi. Tarifa za ukaguzi wa usalama na afya mahala pa kazi zilizopitiwa zilikutwa na tofauti katika maudhui wakati zilipolinganishwa ndani ya kanda na miongoni mwa ofisi za kanda ambayo ilisababishwa na ukosefu wa muundo wa kuandika taarifa ambao ingeweza kutumiwa kama mwongozo kwa wakaguzi wakati wa kuripoti matokeo ya ukaguzi uliofanyika.

Pia ilibainishwa kuwa hakukuwa na tathmini zilizofanyika katika kupima ubora wa ukaguzi uliofanyika ili kuthibitisha kama kazi imefikia viwango vya ubora unaotakikana.

Taarifa za ukaguzi zilizokamilika hazitumwi kwa wakati kwa wajiri kama mrejesho na hazitumiki kama msingi kwa ajili ya kuchukua hatua za marekebicho. Mrejesho juu ya ukaguzi uliofanyika unatolewa kwa

maneno pindi ukaguzi unapokamilika, na kwa hiyo, inakosa kumbukumbu na mapendekezo yaliyopo kimaandishi kwa ajili ya ufuatiliaji hapo badaye.

Ukaguzi wa ufuatiliaji kuthibitisha kama mapendekezo yaliyotolewa kwa waajiri kwa maeneo yaliyo mbali ni nadra kufanyika kutokana na ukosefu wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya kugharimia ufuatiliaji huo.

3.3.4 Uchunguzi wa afya kwa wajiriwa

Wafanyakazi wachache hufanyiwa uchunguzi wa afya mara kwa mara na baada ya kuacha kazi. Kati ya waajiriwa 167 katika maeneo ya kazi 27 yaliyotembelewa, 66% ya wajiriwa hawajafanyiwa uchunguzi wa kiafya wa mara kwa mara wakati asilimia 34 tu ya waajiriwa waliofanyiwa uchunguzi ndani ya kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2009/2010 to 2011/2012.

3.3.5 Kamati za usalama na afya sehemu za kazi

Waajiri wanasita kuunda Kamati za Afya na Usalama kazini katika maeneo yao ya kazi kwa sababu ya hofu kwamba wajumbe wa kamati hizi/ wawakilishi wataripoti ajali na magonjwa na au mazingira duni ya mahala pa kazi kwa OSHA ambayo inaweza kusababisha kuwekewa vikwazo. Kama kamati hizi zingeanzishwa na kufanywa imara na madhubuti, zingeweza kushughulikia jukumu muhimu katika kuhakikisha kwamba hali ya usalama na afya katika maeneo ya kazi kwa kiasi kikubwa inaboreshwa.

3.3.6 Makadirio na hali halisi ya makusanyo

Makadirio katika ukusanyaji wa ada ya usajili ni TSh. 3.176 bilioni wakati makusanyo halisi yaliyokusanywa na OSHA toka maeneo ya kazi ni TShs. 0.664 bilioni sawa na 21%. Vile vile, uwezo wa kukusanya ada ya mwaka ni TSh. 13.156 bilioni wakati kiasi halisi kilichokusanywa ni TShs. 0.92 bilioni sawa na 7%. Mapato mengine yaliyokusanywa na OSHA yametokana na uchunguzi wa ajali TSh. Milioni 2.8 kutoka makosa ni TShs. 80 milioni na tathmini ya vihatarishi ni TShs. 24 milioni. Hii inafanya jumla ya mapato yaliyokusanywa na OSHA kuwa Sh. Milioni 1,691 tu.

3.3.7 Mfumo kuhakiki Mtaji wa uwekezaji

Mapitio ya rekodi za fedha ya ada zilizokusanywa na mahojiano na maofisa wote katika Makao Makuu ya OSHA na ofisi za kanda zimebaini kwamba OSHA haina mfumo wa kuhakiki mtaji wa uwekezaji katika maeneo ya kazi mbalimbali yaliyosajiliwa na kukaguliwa. OSHA hutegemea taarifa (mtaji wa uwekezaji wa maeneo ya kazi tofauti) wanazopewa na waajiri.

3.3.8 Mgawanyo wa rasilimali kwajili ya shughuli za usalama na afya mahali pa kazi

Wizara mama, Wizara ya Kazi na Ajira haijatoa mtaji wa kutosha kwa OSHA ili kuwawezesha OSHA kufanya kazi yake kama vile kubainisha na usajili wa maeneo ya kazi, ukaguzi wa maeneo ya kazi, kufanya ukaguzi wa afya na usalama, ufuatiliaji na tathmini ya afya na athari ya usalama mahali pa kazi.

3.3.9 Ufuatiliaji wa shughuli za afya na usalama mahali pa kazi

Imebainika kwamba Wizara ya Kazi na Ajira haijafanya ufuatiliaji na tathimini zinazohusu shughuli za usalama na afya mahali pa kazi zinazofanyika na OSHA. Wizara haijaandaa vigezo vya kupima utendaji wa shughuli za usalama na afya mahali pa kazi na haina mpango wa Ufuatiliaji na tathimini.

OSHA imekuwa ikifuatilia mapato yaliyokusanywa kulinganisha na ada iliyolipwa katika ukaguzi wa usalama na afya mahali pa kazi, na taarifa za mara kwa mara zinazotumwa na ofisi ya OSHA makao makuu kutoka Ofisi za Kanda. Viashiria vingine muhimu kama vile kiwango waajiri kufuata sheria, asilimia ya malalamiko juu ya masuala ya usalama na afya mahala pa kazi, kiwango cha magonjwa ya kazi na ajali yamepewa tahadhari kidogo. Hata hivyo, hakuna mfumo wa kufatilia ukaguzi uliofanyika.

3.4 Tulichohitimisha

Ukaguzi wetu na matokeo ya tulichokiona umetuongoza kuhitimisha kwamba maeneo ya kazi machache tu (24%) ndio yaliyosajiliwa. OSHA

inakosa mipango maalum kwa ajili ya kubaini maeneo ya kazi ambayo hayajasajiliwa na kuyasajili maeneo ya kazi yaliyobainika. Kaguzi hazipangwi na kufanyika kwa ufanisi. Vilevile, hakukuwa na mfumo wa kuhakikisha ubora wa kaguzi zinazofaywa.

Kamati na wawakilishi wa usalama na afya kazini ambapo zipo hazitekelezi majukumu yao kama inavyotakiwa. Mafunzo hayapangwi na kufanyika ipasavyo. Wizara ya Kazi na Ajira haijafanya tathimini na ufuatiliaji wa utendaji wa OSHA na kaguzi zinazofanyika.

3.5 Tulichopendekeza

3.5.1 Usimamizi wa Usajili maeneo ya kazi

Wakala wa Usalama na afya Mahali pa kazi (OSHA) wanatakiwa:

1. Kuanzisha mkakati kwa ajili ya kubaini na kusajili maeneo ya kazi yote ambayo hayajasajiliwa nchini.
2. Kuchukua hatua kwa maeneo ya kazi yote ambayo hayajasajiliwa na OSHA.

3.5.2 Usimamizi wa ukaguzi wa usalama na afya mahali pa kazi

Wakala wa usalama na afya mahali pa kazi (OSHA) inapaswa kuhakikisha kwamba:

1. Mipango ya ukaguzi ya usalama na afya mahali pa kazi inaboreshwa kwa kuhakikisha kwamba kila ofisi ya kanda inaandaa mipango na utekelezaji unasimamiwa, unaratibiwa na kufuatiliwa na OSHA makao makuu;
2. inaandaa Miwongozo wa kufanya ukaguzi uliojikita katika kuangalia viashira vya hatari na kutumika na wakaguzi wote;
3. kipaumbele cha ukaguzi kiwe katika maeneo ya kazi yenye viashiria vikubwa vya hatari ilikuleta ufanisi matumizi ya rasilimali;
4. Mwongozo juu ya uandaaji taarifa unakuwepo na kutumika. Mwongozo huo unatakiwa kutaja mahitaji ya

- kimsingi katika uandaaji wa tarifa.
5. Ukaguzi wa ufuatiliaji unafanyika mara kwa mara ili kutathmini kiwango cha utekelezaji wa mapendekezo ya awali yaliyotolewa na OSHA kwa maeneo ya kazi yaliyokaguliwa.
 6. Kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) iandae viwango vya usalama na afya mahala pa kazi nchini.

3.5.3 Mafunzo ya usalama na afya mahali pa kazi

Wakala wa usalama na afya mahali pa kazi (OSHA) inapaswa kuhakikisha kwamba:

1. Tathmini ya mahitaji ya kila mahali pa kazi yanafanyika kwa kupitia kaguzi za usalama na afya mahali pa kazi kwa nia ya kubaini mahitaji ya mafunzo yatokanayo na mapungufu yaliyobainishwa wakati wa ukaguzi;
2. Mikakati kwa ajili ya kuwa na mafunzo ya usalama na afya mahali pa kazi yenye gharama nafuu inaandaliwa na kutekelezwa; na
3. Uratibu wa taasisi zote za serikali zinazotoa mafunzo kuhusiana na masuala na afya mahala pa kazi inaimarishwa.

3.5.4 Hifadhidata kwa Masuala ya Usalam na afya mahali pa kazi

Wakala wa usalama na afya mahali pa kazi (OSHA) inapaswa kuhakikisha kwamba:

1. Inaandaa sera rasmi na taratibu ambazo zitatoa maelezo ya ufasaha katika ukusanyaji rekodi na kudumisha kumbukumbu kuhusu ajali na magonjwa wayapatayo waajiriwa mahala pa kazi.
2. Inaweka mfumo kwa ajili ya kuzalisha na kutumia data katika kushughulikia, kufuatilia afya na usalama mahali

- pa kazi na kubaini matatizo.
3. Inaandaa hifadhidata ya kamati ya usalama na afya kazini na wawakilishi waliopo katika maeneo ya kazi, kuainisha waliopata na wasiopata mafunzo na mara kwa mara kutathmini ufanisi wa kamati hizi katika kuboresha masuala ya usalama na afya katika maeneo yao ya kazi.

3.5.5 Usimamizi wa rasilimali za shughuli za usalama na afya mahali pa kazi

Wakala wa usalama na afya mahali pa kazi (OSHA) inapaswa kuhakikisha kwamba:

1. Inaandaa mfumo wa kukusanya mapato yote yaliyopo ndani ya uwezo yanayotokana na usajili, ukaguzi, uchunguzi na vikwazo vilivyowekwa;
2. Inaweka utaratibu wa kuhakiki mtaji uliowekezwa mahali pa kazi; mtaji uliowekezwa uwe ndio msingi kwa ajili ya kukokotoa ada ya ukaguzi na iwe na mabadiliko kama biashara inakua / inashuka; na
3. Inaandaa mfumo wazi kwa ajili ya ugawaji wa rasilimali kwa kuhakikisha kuwa rasilimali muhimu (rasilimali watu, fedha, zana za ukaguzi na magari) zinagawiwa vya kutosha na maeneo yote yenye viashiria vikubwa vya hatari ya ajali na magonjwa yanapewa kipaumbele.

SURA YA NNE

USIMAMIZI WA MIKATABA YA MIRADI YA MAENDELEO KATIKA SERIKALI ZA MITAA

4.1 Tulichochunguza

Sisi tulichunguza kama serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Sekretarieti za Mikoa ina mfumo madhubuti kwa ajili ya kusimamia mikataba ya ujenzi wa miradi ya maendeleo katika Serikali za Mitaa ambayo ili kupunguza ucheleweshaji, ongezeko la gharama na kasoro ya ubora katika miradi ya maendeleo iliyokamilika.

Ili kukabiliana na lengo lililotajwa hapo juu, ukaguzi umezingatia maswali kuu manne kama yalivyoelezwa hapa chini:

Swali la Ukaguzi 1: Je Serikali za Mitaa wanapanga na kubajeti vya kutosha kwa ajili ya miradi ya maendeleo?

Swali la Ukaguzi 2: Je, kuna udhibiti wa kutosha unaofanyakazi kushughulikia ucheleweshaji, kuongezeka kwa gharama na matatizo ya ubora wa miradi ya maendeleo ya ujenzi katika Serikali za Mitaa?

Swali la Ukaguzi 3: Je, mamlaka za juu zaidi (Sekretarieti ya Mkoa (RS) na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI) wanafanya ufuatiliaji wa mara kwa mara na tathmini ya miradi ya maendeleo katika Serikali za Mitaa kitija na kiufanisi?

Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ina majukumu ya jumla kwa ajili ya kutoa miongozo, kufuatilia na kutathmini utendaji wa Serikali za Mitaa. Aidha, wizara sekta kama vile Wizara ya Fedha, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, Wizara ya Afya na Ustawi wa na Jamii, Wizara ya Maji ina wajibu wa kutengeneza sera ya sekta, mipango katika ngazi ya taifa, kutoa msaada kwa Sekretarieti ya Mkoa na Serikali za Mitaa na katika kujenga uwezo wa kiufundi na kuwahakikishia ujenzi bora kupitia uundaji wa viwango na miongozo. Pia kufuatilia, kuhakiki na kutathmini mpango.

4.2 Umuhimu wake

Miradi ya maendeleo katika juhudi za Serikali za Mitaa (SM) katika Tanzania unalenga katika kuboresha huduma kwa wananchi kama vile huduma za afya, elimu na maji. Kulingana na bajeti ya Taifa kwa miaka mitatu ya fedha yaani 2009/10 - 2012/13, bajeti kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Halmashauri ilikuwa kati ya 26% na 36% ya jumla ya bajeti ya taifa. Kuna matatizo mengi yamebainishwa na wadau mbalimbali katika miradi chini ya utekelezaji. Hii ni kama vile miradi kuto kukamilika ndani ya muda waliokubaliana na hivyo kusababisha faida iliyokusudiwa ya mradi kwa umma kuchelewa. Tatizo jingine linahusu kuongezeka kwa gharama - kwa wastani kuanzia kati ya 78%-155% ya gharama ya awali ya mradi - ambayo ilisababisha gharama za ziada ambazo zingeweza kuepukwa ukilinganisha na gharama za awali. Tatizo la tatu linahusu ubora wa miradi ya maendeleo iliyokamilika. Kulingana na ripoti ya utendaji ya mwaka iliyotolewa na PPRA Mwaka 2010/11 uliofanywa katika miradi 136, 64% ya miradi ilikuwa na ubora usioridhisha.

4.3 Tulichokiona

4.3.1 Ukadiriaji muda usio halisi

Wastani wa muda uliokadiriwa wa ajili ya kukamilisha miradi ya maendeleo hauna uhalisia. Kama ilivyoonekana kwamba kuna tofauti kubwa kati ya makadirio ya muda wa mhandisi na wakati halisi uliochukua kukamilisha miradi. Kuna tofauti ya 70% ya makadirio ya mhandisi na wakati halisi. Hii imesababishwa na ukosefu wa kufanya kazi ya uhakika wa kuja na wastani wa muda kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wakati wa hatua ya kupanga. Maafisa wa Serikali za Mitaa hawajafanya jitihada madhubuti kuhakikisha kwamba mradi wowote unaotekelezwa katika halmashauri una makadirio sahihi ya muda ambao utawaongoza wakati wa kumnunua mkandarasi na hata wakati wa kusimamia kazi ya ujenzi.

4.3.2 Ukadiriaji gharama usio halisi

Serikali za Mitaa hazitumii makadirio ya gharama yaliyotolewa na mhandisi wakati wa kuandaa bajeti na kusababisha mabadiliko ya

gharama. Kuna tofauti kubwa kati ya gharama iliyokadiriwa na iliyowekwa katika bajeti. kiasi cha bajeti ni ndogo kulinganisha na makadirio ya gharama ya mradi. Vile vile, gharama ya makadirio ambayo yamekuwa yakitolewa na wahandisi nayo hayana uhalisia, kwani kuna tofauti kubwa kati ya makisio ya gharama ya mradi na gharama halisi zilizotumika baada ya kukamilika kwa mradi huo. Kuna tofauti nyingi na ongezeko la kazi wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hii imesababishwa na kushindwa kwa Halmashauri kuja na makisio yaliyochambuliwa gharama wakati wa hatua ya kupanga.

Pia, makisio ya gharama yamekuwa yakifanyika katika ngazi za juu yaani katika ngazi ya wizara ya sekta. Kwa mfano, kwa MMAM mwongozo wa gharama za mradi wa ukarabati wa vituo huduma za afya ulikuwa Tshs. milioni 14 kwa ajili ya zahanati na milioni 56 kwa ajili ya vituo vya afya. Makadirio haya yalitolewa baada ya utafiti wa nchi nzima na kuamua gharama ya ukarabati wa vituo vya afya kabla ya mradi kuanza.

Lakini makadirio haya ni kielelezo elekezi kwani kunatofauti ya mandhari na udongo katika Serikali za Mitaa mbalimbali katika Tanzania, hivyo kuna haja kwa wahandisi wa halmashauri kufanya makisio ya gharama wakati wa hatua ya kupanga ili kubaini uhalisia kama iwezekanavyo. Jedwali 4.1 hapa chini linaonyesha asilimia ya Serikali za Mitaa ambayo walifanya makisio ya gharama ya mradi katika sekta tatu kwa Halmashauri saba zilizoangaliwa:

Jedwali 4.1: Asilimia ya Halmashauri zilizofanya makadirio ya gharama za mradi katika sekta tulizoangalia

Sekta	% ya Serikali za Mitaa zilizokadiriya gharama	% ya Serikali za Mitaa ambazo hazikukadiriya gharama
Kilimo na Mifugo	71	29
Maji	57	43
Afya	29	71

Chanzo: Uchambuzi wa wakaguzi

Jedwali hapo juu linaonyesha kwamba sekta ya kilimo na mifugo na maji ndiyo walifanya makisio ya gharama ya mradi, wakati sekta ya afya mara chache kufanya makadirio ya gharama katika miradi mingi.

4.3.3 Ukosefu wa uhakika wa ubora katika hatua ya mipango

Halmashauri hawana utaratibu kuhakikishia uhakika wa ubora katika hatua ya mipango kabla ya utekelezaji wa mradi ili kupunguza hatari ya kuwa na miradi ya maendeleo ambayo ni ya ubora wa chini. Kwa mfano imebainika kwamba Halmashauri ya Manyoni haikuwa na mpango kwa ajili ya matakwa ya mradi (vipimo), maabara na jaribio la vipimo na ratiba ya kazi ambayo mifumo yote iliyotajwa hapo juu ni ya muhimu katika kuhakikishia ubora wa miradi ya maendeleo.

4.3.4 Manunuzi ya makandarasi hayapangiliwi ipasavyo na Serikali ya Halmashauri za Mitaa

Ununuzi wa makandarasi haupangiliwi ipasavyo. Wengi wa makandarasi kwa ajili ya miradi ya kilimo na mifugo, afya na maji ya maendeleo walinunuliwa si kulingana na mpango wa mwaka wa manunuzi ulio chini ya utekelezaji. Asilimia ya miradi iliyotekelezwa kinyume na mpango wa manunuzi katika Halmashauri ni kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 4.2 hapa chini:

Jedwali 4.2: Asilimia ya miradi iliyotekelezwa nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka

Halmashauri	Asilimia ya miradi iliyotekelezwa nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka		
	Miradi ya Kilimo na Mifugo	Miradi ya Afya	Miradi ya Maji
Mufindi	100	80	89
Mbinga	60	-	-
Mbeya Jiji	-	100	100
Urambo	83	100	100
Serengeti	100	57	-
Monduli	-	100	100
Manyoni	-	100	100

4.3.5 Uratibu usiotosheleza wakati wa mipango ya miradi ya maendeleo

Ilibainishwa kuwa halmashauri haijatengeneza mpango juu ya jinsi

ya kuratibu shughuli za ujenzi kwa wadau mbalimbali katika maeneo yao. Hii imesababisha baadhi ya miradi ya maendeleo kuchukua muda mrefu kukamilika na mingine kutotekezwa kutokana na Serikali za Mitaa kutowahusisha ipasavyo makampuni ya huduma kwa mfano TANESCO, Mamlaka ya Maji nk, kabla ya kuanza kwa mradi. Kushindwa kuwahusisha wadau muhimu katika hatua ya kupanga kumesababisha ucheleweshaji wa miradi na ongezeko la gharama.

4.3.6 Utekelezaji wa miradi usio wa wakati

Miradi haianzishwi na kukamilika kwa wakati. Kuna ucheleweshaji katika muda wa kuanzisha mradi. Vile vile kuna ucheleweshaji katika kukamilika kwa mradi kwa wakati muda uliopangwa kulingana na mkataba. Hii imebainishwa katika sekta zote tatu zilizokaguliwa. Ucheleweshaji huu umeonekana katika kipindi chote cha ukaguzi (2008/9-2011/12).

Kiwango cha ucheleweshaji (tofauti kati ya muda wa awali na wakati halisi) katika sekta tatu ya kilimo na mifugo, afya na maji ni kama inavyoonekana katika Jedwali 4.3.

Jedwali 4.3: Kiwango cha kuchelewa kukamilika kwa miradi katika sekta tatu zilizokaguliwa

Sekta	Kiwango cha uchelewaji (Miezi)
Kilimo na Mifugo	1 - 14
Afya	34
Sekta ya maji	0.5 - 30

Chanzo: Uchambuzi wa wakaguzi

Matatizo yanayoendana na ucheleweshaji yamechunguzwa kwa kina katika miradi 119 ya ujenzi. Ucheleweshaji umetokana na sababu kama kuhamisha huduma, ukosefu wa uratibu mzuri na serikali za mitaa, ucheleweshaji wa malipo kwa wahisani, muda wa mchakato wa kutoa idhini ya misamaha ya kodi au sababu zilizojitokeza kwa uwezo.

4.3.7 Kuongezeka kwa gharama wakati wa utekelezaji wa miradi

Miradi mingi haikukamilika kwa gharama za mkataba. Hii ilionekana

katika sekta zote tatu zilizokaguliwa. Jedwali 4.4 linaonyesha kiwango cha kuongezeka kwa gharama katika Kukamilika kwa miradi katika Sekta mbalimbali.

Jedwali 4.4: Kiwango cha kuongezeka kwa gharama katika Kukamilika kwa miradi katika Sekta mbalimbali

Sekta	Idadi ya Mradi katika sampuli	Idadi ya miradi iliyoongezeka gharama	Kiwango cha ongezeko la gharama (%)
Kilimo na Mifugo ¹	33	9	9 - 20
Miradi ya afya	36	8	5 - 55
Miradi ya sekta ya maji ²	45	3	1 - 33
Jumla	114	20	

Chanzo: Uchambuzi wa wakaguzi

Kama inavyoonekana hapo juu, gharama kwa miradi ishirini imeongezeka kuanzia 1% hadi 55% kutoka bajeti ya awali. Kwa miradi ya Afya, mabadiliko hayo ni makubwa.

4.3.8 Miradi ya ujenzi kutogharimiwa ipasavyo

Kuna tatizo katika serikali kuu katikakugharamia miradi ya maendeleo katika Serikali za Mitaa kulingana na bajeti iliyopitishwa. Ni kawaida kuona katika miaka minne iliyopita kiwango kilichopitishwa kugharamia ujenzi wa miradi ya maendeleo kutotolewa yote. Kiasi cha fedha kilichotolewa kimeshuka na kuwa karibia 50%, ambayo inamaanisha kuwa ni 50% tu ya miradi iliyopangwa imetekelezwa. Hata hivyo, ingawa kiwango kilichotolewa ni 50%, bado hakikutolewa kwa wakati. Katika Halmashauri nyingi pesa za miradi zilitolewa mwishoni mwa robo ya pili ya mwaka na kiasi kikubwa cha fedha kilitolewa katika robo ya nne.

¹Data za Halmashauri ya Wilaya ya Monduli hazijawekwa (muda wa kukamilisha katika miradi husika haukuchukuliwa)

²Mbeya Halmashauri ya Jiji haikuwa na data

4.3.9 Ukosefu wa mipango ya ufuatiliaji na ukaguzi katika utekelezaji wa miradi

Ilibainishwa kuwa katika Halmashauri zote zilizotembelewa kulikuwa hakuna mipango kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji na usimamizi wa miradi ya ujenzi. Hivyo, katika kipengele cha ufuatiliaji na ukaguzi ni mara chache kufanyika au kutofanyika kabisa. Hata kwa ufuatiliaji na ukaguzi uliofanyika, hakukuwa na malengo ya wazi yaliyolenga maeneo maalumu. Kasoro hii, ya kutokuwa na mipango mizuri katika ufuatiliaji na ukaguzi yamepelekea ugumu kwa halmashauri kufuatilia shughuli za ujenzi katika maeneo ya miradi na kusababisha kushangazwa wakati mradi wa ujenzi unapochelewa, kuwa na gharama kubwa tofauti na gharama iliyo pangwa na pia kuwa katika ubora wa chini.

kutokana na ufuatiliaji na ukaguzi wa miradi kutopewa angalizo ni mara chache shughuli hizo kutengewa fedha katika bajeti. Kiasi pekee kinachotengwa ni kwaajili ya kazi za ujenzi ingawa inajulikana wazi kwamba wakandarasi na washauri hawawezi kufanya kazi nzuri bila kuwa na ufuatiliaji na ukaguzi wa karibu wa miradi utakaofanywa na maafisa wa Serikali za Mitaa.

4.3.10 Upungufu wa msaada kutoka serikali kuu

Kupitia mahojiano na maafisa wa Serikali za Mitaa na mapitio ya nyaraka za miradi, makisio ya mara ngapi aina tofauti tofauti za kusimamia, kufuatilia na ukaguzi wa shughuli zimefanywa na Serikali za Mitaa ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

Jedwali 4.5: Kiwango cha usimamizi wa miradi uliofanywa na maafisa wa halmashauri

Sekta	Shughuli za usimamizi	kiwango		
		yakuridhisha	wastani	Si yakuridhisha
Kilimo na mifugo	Ziara za mwezi katika miradi		√ ³	
	Upimaji wa kazi		√ ⁴	
	Utoaji wa idhini ya kazi baada ya ukaguzi		√ ⁵	
	Utayarishaji wa ripoti			√ ⁶
Afya	Ziara za mwezi katika miradi		√	
	Upimaji wa kazi		√	
	Utoaji wa idhini ya kazi baada ya ukaguzi			√ ⁷
	Utayarishaji wa ripoti			√ ⁸
Maji	Ziara za mwezi katika miradi	√		
	Upimaji wa kazi		√	
	Utoaji wa idhini ya kazi baada ya ukaguzi		√	
	Utayarishaji wa ripoti	√		

Source: Nyaraka za mradi husika - Mawasiliano kati ya maafisa wa halmashauri/ washauri na wakandarasi

³Siyo miradi yote ilitembelewa kila mwezi

⁴Maranyingi inafanyika wakati wa kuthibitisha kwa ajili ya malipo

⁵Siyo idhini zote zilizotolewa zilitunzwa

⁶Baada ya ziara katika mradi na ukaguzi ni ripoti chache ziliandaliwa

⁷Idhini zilizotolewa hazikuhifadhiwa ipasavyo

⁸Baada ya ziara katika mradi na ukaguzi ripoti haikuandaliwa

Kama inavyoonekana hapo juu usimamizi wa miradi kwa Serikali za Mitaa haukufanyika vya kutosha katika sekta zote tatu zilizokaguliwa. Ni ukaguzi wa miradi na upimaji wa kazi tu ndiyo uliofanywa kwa wastani, hata hivyo, siyo miradi yote ilikaguliwa. Kutokana na mahojiano na wahandisi, wakuu wa idara kwa miradi husika na maafisa wa mipango kutoka katika halmashauri saba, sababu za kuwa na usimamizi duni ni pamoja na: Ukosefu wa mpango mpana wa usimamizi, rasilimali zisizotosheleza katika suala la wafanyakazi wa kiufundi na usafiri usiotosheleza unaohitajika kwa ajili ya kufanya ziara ya mara kwa mara na ukaguzi wa kazi, na ukosefu wa uratibu mzuri kati ya wakuu wa idara wa Serikali za Mitaa na Idara ya Uhandisi.

4.3.11 Miongozo na majukumu yasiyo wazi katika kufanya ufuatiliaji wa miradi

Ilibainishwa kuwa TAMISEMI haijatengeneza miongozo ya jinsi ya kufuatilia na kusimamia miradi ya ujenzi. Miongozo ingesaidia maafisa wa Serikali za Mitaa na Sekretarieti ya Mkoa kuelewa wazi jinsi gani wanatakiwa kupanga, kufanya na kutoa taarifa kwa kuzingatia aina ya mradi. Udhaifu mwingine ni katika kuelezea wajibu wa wadau mbalimbali wanaohusika katika kufuatilia. Haiko wazi majukumu ya idara ya Uhandisi na mipango katika ufuatiliaji wa miradi. Kasoro hii imesababisha ufuatiliaji dhaifu na kuwepo kwa ukaguzi wa dharura.

4.3.12 Idadi nyingi ya miradi iliyopangwa kutekelezwa ukilinganisha na fedha zilizoidhinishwa

Ilibainishwa kuwa, Serikali za Mitaa huwa na idadi kubwa ya miradi iliyopangwa ambayo kwa hakika ni aidha inayoendelea (ambayo haijakamilika au kumalizika nusu) kwa muda mrefu kabisa yaani hadi miaka mitatu ya fedha au bado kuanza kabisa.

Ukaguzi ulibainisha kuwa miradi ya maendeleo yote iliyochini ya sekta hizi tatu za afya, maji na kilimo na mifugo, tatizo la kuwa na miradi mingi ukilinganisha na bajeti iliyopo ni kitu cha kawaida.

4.3.13 Usanifu usiotosheleza wa miradi ya ujenzi

Ilibainishwa kuwa kuna udhaifu mkubwa katika usanifu wa miradi ya

ujenzi katika sekta zote tatu ambapo utafiti ulifanywa na timu ya ukaguzi. Hii inahusishwa na michoro ya kiwango na 'BOQ' iliyotayarishwa na wizara husika yaani ya Afya na Ustawi, Maji na Umwagiliaji, Kilimo na Chakula na Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Michoro iliyotengenezwa haikuweza kutosheleza mahitaji ya Serikali za Mitaa tofauti na watumiaji. Hii ni kwa sababu wizara husika imetengeneza mchoro mmoja kutumika nchi nzima wakati inajulikana kwamba Tanzania ni nchi kubwa yenye maeneo yenye tofauti kubwa ya hali ya hewa, mahitaji, utamaduni nk.

kupitishwa kwa 'BOQ' zilizotengenezwa na wizara bila kuziweka ziendane na hali halisi kumesababisha gharama za ziada wakati wa utekelezaji wa miradi. Gharama hizi za ziada ni matokeo ya kutozingatia mambo kama vile hali ya udongo, ardhi na eneo kijiografia nk. Gharama ya ziada ambayo baadaye ilisababisha ongezeko la gharama la mradi ambazo zingeweza kushughulikia mapema kama halmashauri ingechukua jitihada kuweka michoro sanifu katika kiwango cha uhalisia na kufanya mapitio ya 'BoQ'. walimwita kama overrun gharama inaweza kutafutiwa ufumbuzi mapema iwapo Serikali za Mitaa inaweza kuchukua hatua ya customizing michoro sanifu na mapitio BOQ ipasavyo.

4.4 Tulichohitimisha

Kwa ujumla, ofisi za ukaguzi imehitimisha kwamba mfumo wa kusimamia mikataba ya ujenzi wa miradi ya maendeleo katika Serikali za Mitaa si ya ufanisi. Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Sekretarieti za Mikoa hawajaweza kufuatilia na kutathmini vya kutosha utekelezaji wa miradi ili kupunguza ucheleweshaji, ongezeko la gharama na kasoro za ubora katika miradi ya maendeleo iliyokamilika. Upimaji ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo katika Serikali za Mitaa haufanyiki kwa ufanisi na mamlaka ya juu ya serikali (TAMISEMI/Wizara ya Fedha).

Halmashauri hazijaweza kupanga na kubajeti vya kutosha miradi ya maendeleo. Kuchelewa, kuongezeka kwa gharama na masuala ya ubora hayajashughulikiwa vya kutosha na Serikali za Mitaa na mamlaka nyingine za juu zinazohusika.

4.5 Tulichopendekeza

Kulingana na matokeo ya ukaguzi na hitimisho tulipendekeza kama ifuatavyo:

4.5.1 Mipango na Bajeti kwa miradi ya maendeleo

Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inapaswa kuhakikisha kwamba:

- Idadi ya miradi ya ujenzi iliyopangwa inagharamiwa ipasavyo na serikali kuepuka kuwa na miradi mingi ambayo serikali haiwezi kugharamia;
- Utolewaji wa fedha unafanyika kwa wakati na kulingana na bajeti iliyoidhinishwa inayotokana na mtiririko wa fedha wa halmashauri;
- Makisio ya muda wa kumaliza na gharama kwa miradi ya ujenzi yaha uhalisia iwezekanavyo na taarifa husika ya mradi zitumike katika kubajeti, kumnunua mkandarasi na kusimamia miradi;
- Usanifu wa miradi ya ujenzi ifanyike kikamilifu na kiuchumi ili kufikia mahitaji ya walengwa husika;
- Mipango ya manunuzi ya mwaka iwe na uhalisia; na pia kuhakikisha manunuzi ya wakandarasi/washauri yanafanyika kulingana na mpango wa manunuzi wa mwaka;
- Serikali za Mitaa zinasimamia ipasavyo mchakato wa manunuzi katika ngazi ya kata na pia tathmini ifanyike kuwachambua wakandarasi ili kuepuka kumtumia mkandarasi mwenye uwezo mdogo katika miradi ya ujenzi; na LGAs are adequately supervising the procurement process at the ward level

- Wanatoa maelekezo ya wazi / miongozo ambayo itakuwa mwongozo wa Serikali za Mitaa katika siku zijazo kwa ajili ya miradi ya ujenzi. Mwongozo lazima ueleze kwa kina vigezo vya kuchukuliwa wakati wa kuamua juu ya idadi ya miradi ya kutekelezwa katika mwaka wa fedha husika ili kuepuka kuwa na miradi mingi midogo ambayo haiwezi kukamilika kwa wakati na kusambaza rasilimali fedha chache iliyopo kati ya miradi mingi.

4.5.2 Utekekezaji wa miradi ya maendeleo

Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inapaswa kuhakikisha kwamba:

- Wanaweka mifumo ambao utahakikisha Halmashauri wanadhibiti muda, gharama na ubora wa miradi yao ya ujenzi.

4.5.3 Ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo

Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inapaswa kuhakikisha kwamba:

- Wanatengeneza mwongozo juu ya Usimamizi na Ufuatiliaji wa miradi ya ujenzi ili kusaidia TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara, usimamizi na utoaji taarifa ya maendeleo katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi katika Serikali za Mitaa;
- Ufuatiliaji na Usimamizi wa miradi ya ujenzi katika serikali za mitaa ni unafanyika vizuri na ripoti inatolewa, matokeo na mapendekezo yanatekelezwa ipasavyo; na
- Bajeti kwa ajili ya ufuatiliaji na usimamizi wa kila mradi wa ujenzi inatengwa.

SURA YA TANO

USIMAMIZI WA UNUNUZI WA VIFAA TEHAMA KATIKA SEKTA YA UMMA

1.1 Tulichokichunguza

Lengo la ukaguzi ilikuwa kutathmini kiwango ambacho mamlaka husika zimefanya ufuatiliaji na tathmini juu ya manunuzi ya umma na iwapo hatua sahihi zimechukuliwa ili kuboresha namna ambavyo mfumo wa manunuzi unafanya kazi.

Ukaguzi ulitazama kiwango cha ufanisi katika usimamizi wa manunuzi kwa kuangalia yafuatayo: tathmini ya mahitaji ya watumiaji; uwekaji wa viwango vya ubora; udhibiti wa ubora; na ufuatiliaji na tathmini unaofanywa na mamlaka za juu. Ukaguzi ulilenga katika usimamiaji wa manunuzi ya vifaa vya TEHAMA hasa kompyuta (desktop na Laptop), mashine za uchapishaji (printers), na mashine za kutolea nakala (scanners).

Mkaguliwa mkuu katika ukaguzi huu ni Wizara ya Fedha hasa kupitia Idara ya Sera za Manunuzi ya Umma (PPD). Ukaguzi ililenga serikali kuu na hasa Wizara 4 (nne). Taarifa zilizopatikana kutoka Wizara nne zilizochaguliwa zimetumika kuonyesha udhaifu katika utekelezaji wa mfumo uliopo wa ufuatiliaji. Wizara hizo ni: Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Wizara ya Mambo ya Ndani; Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; na Wizara ya Viwanda na Biashara.

Aidha, kutokana na nafasi yake katika udhibiti wa manunuzi ya umma, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ilitumika kama moja ya vyanzo vikuu vya taarifa wakati wa ukaguzi. Wakala wa Huduma ya Manunuzi ya Serikali (GPSA), kwa sababu ya nafasi yao katika kushughulikia manunuzi vitu na huduma kwa kwa taasisi za umma kupitia utaratibu wa mikataba maalum. Taarifa nyingine zilipatikana katika Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ambayo ni mhusika muhimu katika usimamizi wa vifaa vya TEHAMA.

5.2 Umuhimu wake

Matumizi ya Serikali ya Tanzania katika manunuzi ni kati ya 41% na 70% ya bajeti yake ya jumla ya mwaka. Hivi sasa, miongoni mwa vipaumbele vya serikali, pamoja na mambo mengine, ni kuboresha usimamizi katika manunuzi ya umma. Hali hii imetokana na mtazamo wa jumla juu ya matumizi ya ufujaji yanayofanywa na Wizara, Idara na Wakala kupitia manunuzi ya mali na huduma mbalimbali.

Aidha, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wadua mbalimbali kuhusiana na ukubwa wa bei pamoja na bidhaa kuwa za viwango viwango duni pale ambapo bidhaa hununuliwa na vyombo vya umma. Bidhaa hizi hutumika kwa kipindi cha muda mfupi ikilinganishwa na matumizi yaliyotarajiwa ingawa bei yake ni ya juu. Pia bidhaa zimekuwa zikikununuliwa kwa misingi ya manunuzi ya dharura bila ya kuwepo sababu za msingi za kuhalalisha dharura. Masuala haya ndiyo yaliyopelekea kufanyika kwa ukaguzi huu.

5.3 Tulichokiona

5.3.1 Ukadiriaji wa Mahitaji na uwekaji wa Viwango vya Ubora

Taasisi za Manunuzi hazikufanya ipasavyo ukadiriaji wa mahitaji ingawa watumiaji wamekuwa na ushawishi juu ya vitu vilivyonunuliwa. Taasisi zimenunua vifaa vyenye uwezo wa kufanya kazi kubwa wakati ambapo mahitaji halisi ni madogo. Kwa sababu hii vifaa vilivyonunuliwa vimeshindwa kutumika ipasavyo na hivyo muda mwingi kukaa bure.

Viwango vya ubora wa bidhaa ambavyo hutumiwa na Taasisi mbalimbali za Manunuzi vinatofautiana sana. Kila taasisi imekuwa ikiandaa yenyewe viwango vyake.

Wizara ya Sayansi na Teknolojia haijawahi kuanzisha na kuratibu mahitaji na viwango vya ubora kwa vifaa vya TEHAMA. Ukosefu wa uratibu wa mahitaji na viwango vya ubora umesababisha kila Taasisi ya Manunuzi kuwa na viwango vyake vya ubora wa vitendea kazi ingawa matumizi yaliyokusudiwa ya vitendea kazi hivi yanalingana.

5.3.2 Kutofautiana kwa bei za Vifaa vya TEHAMA

Taasisi za Manunuzi hazikuzingatia vikomo vya bei vilivyowekwa na Wakala wa Ununuzi (GPSA), wakala mwenye jukumu kuandaa utaratibu wa kufanya manunuzi ya mali na huduma kwa ajili ya taasisi za serikali.

Taasisi za Manunuzi zimetumia utaratibu wa nukuu za bei (quotations) wakidai kwamba viwango vya ubora vilivyowekwa na GPSA vimepitwa na wakati na kwamba bei kikomo ziliyowekwa na GPSA ni za juu sana. Mapitio ya nyaraka yameonesha kuwa katika 2/3 ya manunuzi ambayo hayakuzingatia maelekezo ya GPSA, bei silizotumika zilikuwa kubwa zaidi ya bei kikomo zilizowekwa na GPSA ingawa viwango vya ubora wa vifaa vilivyounuliwa ulikuwa sawa.

5.3.3 Udhhibiti wa Ubora katika Ununuzi wa vifaa vya TEHAMA

Taasisi za Manunuzi hazikufanya ukaguzi wa vifaa vya TEHAMA wakati wa kuvipokea. Wakaguzi hawakuweza kuona ripoti za ukaguzi zinazohibitisha ya kuwa bidhaa zilizonunuliwa zina ubora uliokusudiwa. Hali hii ilionekana katika taasisi tatu kati ya nne ya zilizokaguliwa. Katika hali hii tasisi zlizofanya manunuzi haziwezi kuwa na uhakika kwamba vifaa vilivyounuliwa vilikidhi viwango vya ubora vilivyokusudiwa.

5.3.4 Utoshelevu mipango, zana na ripoti za ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Taasisi za Manunuzi

Taasisi za Manunuzi zinapaswa kuwa na mipango ya kutosha kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wao wenyewe katika masuala ya manunuzi. Mapitio ya nyaraka yameonesha kuwa taasisi zina mipango ya kuendeleza, kufuatilia na kutathmini utendaji wao kwa ujumla, lakini imetoa kipaumbele kidogo kwa masuala ya manunuzi.

Aidha, mapitio ya nyaraka na mahojiano na maofisa wa taasisi zilizokaguliwa umebaini kuwa taasisi hizo hazijaandaa nyenzo zitakazosaidia katika kufanikisha ufuatiliaji wa wauzaji. Matokeo yake, hakuna ripoti zozote ambazo zimeandaliwa ili kutoa taarifa juu ya utendaji wasambazaji mbalimbali wa vifaa waliotoa huduma kwa

taasisi husika.

5.3.5 Kufanya ufuatiliaji wa utendaji wa wauzaji

Taasisi za manunuzi zinatarajiwa kufanya mapitio ya mara kwa mara wa utendaji wa wauzaji kwa shabaha ya kuangalia malengo na viwango vya ubora vya utendaji katika mikataba ambayo taasisi hizi huingia. Mahojiano yaliyofanyika na maafisa wa taasisi za manunuzi yalionesha kuwa taasisi hizi zimekuwa zikifanya shughuli hii ya ufuatiliaji na matokeo yake yamekuwa yakitolewa taarifa katika ripoti ya mwaka za utendaji. Hata hivyo, mapitio ya ripoti hizi za utendaji za kila mwaka yameonesha kuwa ripoti hizi hazikugusia masuala ya utendaji wasambazaji.

Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa taasisi za manunuzi hazikufuata kikamilifu masharti ya mikataba wakati wa kusimamia utekelezaji wa mikataba husika ya usambazaji. Baadhi ya wauzaji walichelewa katika kutoa bidhaa lakini taasisi hizi hazikuwatoza wasambazaji hawa tozo za ucheleweshaji (liquidated damages) kama ilivyoelezwa katika mikataba.

Aidha, taasisi za manunuzi na hazikufanya walakuweka kwenye kumbukumbu tathmini ya utendaji wauzaji wao katika utekelezaji mikataba ya usambazaji wa vifaa ambavyo taasisi hizi zimenunua. Tathmini pekee ambazo kwa kawaida zimekuwa zikifanyika na taasisi hizi zilihusu uchambuzi wauzaji walioomba kuuza bidhaa zao kwa taasisi husika wakati zabuni.

5.3.6 Mipango ya Wizara ya Fedha kuhusu ufuatiliaji wa mfumo wa manunuzi

Mapitio ya mpango-mkakati wa Wizara yalionyesha wazi kwamba Wizara, kupitia Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPD), ilikuwa na mipango kwa ajili ya: kutunga sera; kuandaa miongozo ya manunuzi itakayotumiwa na taasisi za umma; kuandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa masuala ya manunuzi nchini; kujenga uwezo wa wataalamu wa manunuzi; kufanya tafiti juu ya masuala ya manunuzi katika sekta ya umma ili kuboresha utendaji.

Pamoja na kuwa moja ya majukumu yao, Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPD) hakijajumuisha suala la ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa manunuzi miongoni mwa vipaumbele vyao

ambavyo vingepawsa kutekelezwa katika miaka mitatu iliyopita.

5.3.7 Utunzi wa Sera ya Taifa ya Manunuzi

Utekelezaji wa shughuli hii ulipangwa tangu 2009 na ulitarajiwa kukamilika Juni 2012. Kazi haikukamilika katika kipindi cha miaka mitatu kama ilivyopangwa. Hata hivyo PPD ilifanikiwa kukamilisha rasimu ya sera hiyo na mwezi Desemba 2012 na kuisambaza kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kutoa maoni yatakayoiboresha rasimu hii. Jumla ya fedha zilizotumika kwa ajili ya shughuli hii ni Sh. Bilioni 6.8 hadi kufikia Juni 2012.

5.3.8 Maandalizi ya Miongozo ya Manunuzi kwa Taasisi za Umma

Kulingana na mahojiano yaliyofanyika na maofisa wa PPD pamoja na mapitio ya nyaraka mbalimbali imeonekana kuwa miongozo hii haijaandaliwa hadi sasa. PPD imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya shughuli hii kwa miaka yote tangu 2009 lakini bado shughuli haijawahi kutekelezwa. Kiasi cha fedha kilichotumika katika miaka hiyo mitatu ni TSh. Milioni 228.4.

5.3.9 Kuanzishwa kwa mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Sera ya Manunuzi

Mapitio ya bajeti na ripoti za mwaka za utekelezaji vilionyesha kwamba, kwa miaka mitatu mfululizo, PPD ilitenga fedha kwa ajili ya ufuatiliaji wa namna sera ya manunuzi inatekelezwa. Shughuli hii isingewezekana kutekelezwa kwa kuwa sera yenyewe ambayo inapaswa kutekelezwa haipo. Hata hivyo, PPD imetumia jumla ya TSh milioni 164.7 zilizotengwa kwa ajili ya shughuli hii ya usimamizi katika kipindi cha miaka mitatu kwa kazi nyingine ya kusasisha hifadhidata wataalam wa manunuzi.

5.4 Tulichohitimisha

Matokeo ya ukaguzi huu, kama yalivyoainishwa katika sehemu iliyopita, yametufanya kufikia zifuatazo:

5.4.1 Uanzishwaji wa mahitaji ya manunuzi na viwango vya ubora

Ingawa watumiaji walikuwa na ushawishi juu ya vitu vilivyokuwa

vikinunuliwa, uanzishwaji wa haja ya manunuzi ya vitu vile haukufanyika kwa utoshelevu. Matokeo yake, Taasisi za Manunuzi zimejikuta zikinunua vifaa zaidi kuliko mahitaji halisi na hatimaye vifaa hivyo kufanya kazi ndogo kuliko uwezo wake halisi.

Wizara inayohusika na masuala ya TEHAMA, MCST, ina haijaandaa sifa na viwango vya ubora kwa ajili ya bidhaa mbalimbali za TEHAMA. Wizara hii pia haijaandaa viwango au miongozo kwa ajili ya kuongoza Taasisi za Manunuzi wakati wanataka kununua vifaa vya TEHAMA. Ukosefu wa uratibu juu wa sifa na viwango vya ubora kwa ajili ya bidhaa za TEHAMA kumesababisha kila Taasisi ya Manunuzi kuwa na sifa na viwango vyao wenyewe ingawa na matumizi ya vifaa hivi kwa taasisi hizo yanalingana.

5.4.2 Udhhibiti wa bei za vifaa vya TEHAMA

Kumekuwa na mabadiliko makubwa ya bei za vifaa vya TEHAMA vinavyonunuliwa na taasisi mbalimbali ingawa pamoja na kuwa vifaa hivi vinafanana kwa sifa na viwango na vimenunuliwa katika kipindi kimoja. Hii inaonesha kutokuwepo kwa udhibiti mzuri wa bei za vifaa hivi.

Wakala wa Ununuzi (GPSA), katika kujaribu kudhibiti mabadiliko makubwa ya bei, iliandaa orodha ya vifaa vya matumizi ya kawaida katika taasisi za umma ikiambatana na bei kikomo za vifaa hivyo. Orodha hii ya wauzaji na bei kikomo zilipaswa kufuatwa na taasisi zote za umma. Hata hivyo, baadhi ya taasisi za manunuzi hazikufuata maelekezo haya na kununua vifaa hivyo kwa bei ya juu zaidi.

5.4.3 Udhhibiti wa Ubora katika Ununuzi wa vifaa vya TEHAMA

Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa kushindwa kudhibiti na kuratibu viwango vya ubora wa vifaa vya TEHAMA kumwsababisha baadhi ya Taasisi za Manunuzi kununua vifaa vya gharama kubwa wakati ambapo vifaa mbadala vya gharama nafuu na ubora wa kuridhisha.

Kamati za ukaguzi na mapokezi ya vifaa katika Taasisi za Manunuzi zimeshindwa kutekeleza kikamilifu majukumu yake na kushindwa kutoa taarifa juu ya ubora wa vifaa vilivyopokelewa katika taasisi zao.

5.4.4 Kufanya ufuatiliaji wa utendaji wauzaji

Taasisi za manunuzi hazina mipango ya kufanya mapitio ya utendaji wa wauzaji kuanzia wakati wa kuwapata hadi wakati wa usambazaji wa vifaa husika. Taasisi za manunuzi hazifuati baadhi ya vipengele katika mikataba kama vile tozo za ucheleweshaji (liquidated damages) pale ambapo wauzaji walishindwa kufikisha vifaa kwa wakati uliokubalika katika mikataba husika.

Aidha, taasisi za manunuzi na hazikufanya wala kuweka kwenye kumbukumbu tathmini ya utendaji wauzaji wao katika utekelezaji mikataba ya usambazaji wa vifaa ambavyo taasisi hizi zimenunua. Kwa sababu hii, wauzaji ambao hawakutekeleza majukumu yao kikamilifu waliendelea kupata kazi katika taasisi nyingine.

5.4.5 Usimamizi na tathmini zinazofanywa na Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPD)

Pamoja na kuwa moja ya majukumu yao, Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPD) hakijajumuisha suala la ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa manunuzi miongoni mwa vipaumbele vyao ambavyo vingepawasa kutekelezwa katika miaka mitatu iliyopita. Kutofanyika kwa ufuatiliaji na tathmini ya utendaji katika manunuzi kumeinyima Serikali fursa ya kujifunza kutokana na uzoefu kwa lengo la kuboresha utendaji katika manunuzi ya umma.

Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPD) kimeshindwa kuandaa sera ya taifa ya manunuzi ndani ya miaka mitatu kama ilivyopangwa. Wakati huohuo, kwa miaka mitatu mfululizo kitengo hiki kimetumia fedha za ufuatiliaji na tathmini ya utendaji katika mfumo wa manunuzi hivyo kufanya kazi hii iliyopangwa kutotekelezwa.

Kwa namna hiyohiyo, PPD imeshindwa viwango vya utendaji ili kuzisaidia taasisi za umma zinapofanya manunuzi.

5.5 Tulichopendekeza

Matokeo ya ukaguzi pamoja na hitimisho vimeonesha mapungufu katika kufanya usimamizi na tathmini ya mfumo wa manunuzi

katika Taasisi za Manunuzi pamoja na taasisi za kitaifa za usimamizi. Mapungufu mengine ni katika ukadiriaji wa mahitaji na viwango vya ubora, pamoja na uhibitaji wa gharama na ubora.

Sehemu hii ya ripoti ina mapendekezoyanayoelekezwa kwa Wizara aya Fedha na Taasisi za Manunuzi yanayolenga kushughulikia mapungufu yaliyojitokeza. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inaamini kuwa mapendekezo haya yanapaswa kufikiriwa na kufanyiwa kazi ili kuboresha usimamizi wa manunuzi na kuhakikisha kuwa matumizi ya rasilimali za imam yanaleta thamani halisi.

5.5.1 Uanzishwaji wa mahitaji ya manunuzi na viwango vya ubora

Wizara ya Fedha ihakikishe kuwa:

1. Katika Taasisi za Manunuzi, tathmini ya mahitaji halisi ya vifaa inafanyika kwa kuwashirikisha watumiaji na kuzingatia uwezekano wa vifaa hivyo sambamba na vifaa vilivyopo (compatibility).
2. Katika Taasisi za Manunuzi, wataalamu wa TEHAMA waliomo ndani ndani ya Taasisi za Manunuzi au walioko katika wizara inayohusika na usimamizi wa masuala ya TEHAMA wanatumika vema katika kuandaa viwango vya ubora kwa ajili ya vifaa vya TEHAMA.
3. Katika Taasisi za Manunuzi, mashine kubwa za kuchapisha na kutoa nakala zinatumiwa na watumiaji wengi kadiri ya uwezo wa mashine husika ili mashine hizi zisikae bure.
4. Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia inapaswa kuandaa viwango vya ubora wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya matumizi ya Taasisi za Manunuzi ili kuleta ulinganifu kwa taasisi hizo.

5.5.2 Uhibitaji wa bei za vifaa vya TEHAMA

Wizara ya fedha ihakikishe kuwa:

1. Taasisi za Manunuzi, zinafuata miongozo inayotolewa na Wakala wa Ununuzi (GPSA) katika masuala ya manunuzi kadiri inavyowezekana.

2. Taasisi ya Manunuzi zihakikishe kuwa viwango vya ubora pamoja na uwezo wa vifaa vinavyonunuliwa unazingatia mahitaji halisi ya watumiaji ili kuepuka manunuzi ya vifaa vya gharama kubwa vyenye uwezo mkubwa kuliko mahitaji halisi.

5.5.3 Udhhibiti wa Ubora katika Ununuzi wa vifaa vya TEHAMA

Wizara ya fedha ihakikishe kuwa katika:

1. Taasisi za Manunuzi ukaguzi unafanyika kikamilifu kwa vifaa vinavyopokelewa na taarifa za ukaguzi zinaandaliwa na kiwasilishwa kwa mamlaka husika ili kuhakikisha kuwa vifaa vilivyonunuliwa vina ubora na uwezo uliokusudiwa.
2. Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia hakikishe kuwa inatekeleza majukumu yake ya kudhibiti na kuratibu viwango vya ubora wa vifaa vya TEHAMA ili kuleta tija katika matumizi ya vifaa hivyo.

5.5.4 Kufanya ufuatiliaji wa utendaji wa wauzaji

Wizara ya fedha ihakikishe kuwa:

Taasisi za manunuzi zinafanya usimamizi na tathmini ya utendaji wa mifumo yao ya manunuzi pamoja na utendaji wa wauzaji kwa kuzingatia yafuatayo:

- Taasisi za manunuzi ziandae mipango ya kufanya mapitio ya utendaji wa wauzaji kuanzia wakati wa kuwapata hadi wakati wa usambazaji wa vifaa husika.
- Taasisi za manunuzi zizingatie vipengele katika mikataba kama vile tozo za ucheleweshaji (liquidated damages) pale ambapo wauzaji watahondwa kufikisha vifaa kwa wakati uliokubalika katika mikataba husika.
- Taasisi za manunuzi ziandae ripoti juu ya tathmini ya utendaji wauzaji wao katika utekelezaji mikataba ya usambazaji wa vifaa ambavyo taasisi hizi zimenunua. Tunapendekeza kuwa ripoti hizi zipelekwe kwa Mamlaka ya Manunuzi (PPRA) ambako zitaunganishwa

nakuzifanya ziweze kufikiwa na taasisi zote za manunuzi ilizivasaidie katika kutambua wauzaji ambao hawakuwa na rekodi nzuri za utendaji katika mikataba iliyotangulia ili kuziepusha taasisi hizi kuingia mikataba na wauzaji wasiofaa.

5.5.5 Usimamizi na tathmini zinazofanywa na Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPD)

Wizara ya fedha inapaswa kuhakikisha kuwa:

1. Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPD) kinakamilisha shughuli zilizopangwa kutekelezwa. Shughuli hizo ni pamoja na:
 - i. Maandalizi ya Sera ya Taifa ya Manunuzi; na
 - ii. Maandalizi ya miongozo ya manunuzi kwa ajili ya matumizi ya taasisi za umma wakati wa kufanya manunuzi.

Wizara ya fedha inapaswa kuhakikisha kuwa:

2. Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPD) pia kina jumuishwa kwenye mipango yake pamoja na kutekeleza yafuatayo:
 - i. Kuandaa mpango wa usimamizi na tathmini ya utendaji wa mfumo wa manunuzi; na
 - ii. Kuacha kutumia fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli moja kwa kutekeleza shughuli nyingine na kuhakikisha kuwa shughuli zilizopangwa zinatekelezwa kikamilifu.

SURA YA SITA

UKAGUZI WA USIMAMIZI WA UVUVI KATIKA ZIWA VICTORIA

6.1 Tulichokichunguza

Kupungua kwa kiwango cha samaki aina ya sangara katika Ziwa Victoria ni moja ya masuala katika nchi za Afrika Mashariki yanayopewa umuhimu. Katika miaka ya hivi karibuni, Ziwa Victoria limekabiliwa na uvuaji wa sangara na aina nyingine ya samaki kupita kiwango, Uvuvi kupita kiwango miongoni mwa facta nyingi, unathibitishwa na mwenendo wa kupungua kwa upatikanaji wa sangara na wastani wa urefu unaotakiwa kwa sangara kuvuliwa.

Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ina wajibu wa kuandaa, kutekeleza, kupelemba (ufuatiliaji) na kupitia marekebisho ya muundo wa sera na kanuni za uvuvi Tanzania. Pia, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) hutekeleza sera hizo kupitia halmashauri husika.

Lengo la ukaguzi ni kuchunguza kama Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi (MLFD) imeratibu, dhibiti uvuvi haramu na kufanya doria kwa ufanisi na tija ili kukabiliana na tatizo la uvuvi wa sangara uliopita viwango (Overfishing) katika Ziwa Victoria. Ukaguzi ulitumia taarifa za kipindi cha miaka mitatu kuanzia Juni 2008 hadi December 2011. Pia taarifa zilikusanywa kutoka wilaya 15 zenye shughuli za uvuvi katika mikoa ya Mwanza, Kagera na Mara.

6.2 Umuhimu wake

Uvuvi katika Ziwa Victoria ni shughuli kubwa ya kiuchumi na chanzo muhimu cha mapato kwa jamii husika na makampuni ya kibiashara. Hali halisi ni kwamba, jamii inayoishi kando ya Ziwa Victoria inategemea uvuvi kama shughuli kuu za kiuchumi.

Licha ya umuhimu huo, kiwango cha samaki kinachotakiwa kubaki ziwani kimepungua kupita kiasi kwa miongo kadhaa. Tathmini ya kiasi cha samaki kinachotakiwa kubaki ziwani iliyofanywa na taasisi ya Uvuvi Ziwa Victoria (LVFO) inaonyesha mwenendo wa kupungua kwa samaki

aina sangara tangu mwaka 2000. Kiwango cha chini cha samaki aina ya sangara upande wa Tanzania kinachotakiwa ziwani kinakadiriwa kuwa takriban ya tani 391 katika eneo la kilomita za mraba 35,088 upande wa Tanzania wakati huo huo hazina ya sangara imekuwa ikipungua kupita kiasi kinachotakiwa kwa uvuvi endelevu. Kiwango hicho inakadiriwa kuwa tani 200.

6.3 Tulichokiona

6.3.1 Udhhibiti wa shughuli za Uvuvi katika Ziwa Victoria

Kiwango cha samaki kipo chini ya kiwango kilichopendekezwa. Mwaka 2011, Jumla ya kiasi cha sangara kilichokuwapo upande wa Tanzania inakadiriwa kuwa tani 165,439 na kiasi kinachotakiwa kubaki kwa uvuvi endelevu (kuendeleza kizazi) ni tani 64,141. Wakati kasi ya uvuaji wa sangara kwa mwaka inakadiriwa kuwa tani 101,298 ambapo imezidi kiasi cha tani ambazo zinazotakiwa kubaki kwa uvuvi endelevu.

Ukaguzi umeona kuwa, kuna kiasi kikubwa cha wavuvi na vyombo vya uvuvi havijasajiliwa. 50% ya wavuvi na vyombo vya uvuvi katika Ziwa Victoria havikusajiliwa. Hii ni kutokana na hatua duni zilizochukuliwa ili kudhibiti kiasi cha sangara wanaovuliwa.

Pia ilibainishwa kuwa hakuna kiwango kilichowekwa kwa ajili ya uvuaji wa samaki / sangara kwa mwaka, kwa sababu ya aina ya uvuvi unafanyika Ziwa Victoria ambao ni uvuvi mdogo mdogo “artisanal fishing” ambao umechangia wizara kushindwa kuweka kiwango cha uvuaji. Pia hakukuwa na kumbukumbu zinazoonyesha uratibu na ufuatiliaji wa karibu unaofanywa na maafisa uvuvi wa wilaya pamoja na kikosi doria kudhibiti shinikizo katika uvuaji wa sangara. Vilevile, hakukuwa na mfumo madhubuti kwa sehemu ya Uvuvi udhibiti na doria (MCS unit) na halmashauri kuhakikisha kuwa wavuvi wanatumia zana za uvuvi zilizokubaliwa kisheria na kudhibiti matumizi ya nyavu zenye macho madogo ambayo yameongezeka kwa kasi mwaka 2011.

6.3.2 Uratibu/Ufuatiliaji wa Shughuli za Uvuvi

Ufuatiliaji wa karibu na ukaguzi wa shughuli za uvuvi

Imeonekana kuwa vikundi vya usimamizi wa mialo “Beach

Management Unit (BMU)” vina uwezo mdogo wa kugundua uvuvi haramu, usioripotiwa na kudhibitiwa. Hii ni kutokana kutoweka mipango ya jinsi ya kuendesha shughuli za uvuvi, kutopewa ushirikiano na halmashauri husika and wizara kutofanya tathmini ya kutosha ya maendeleo ya BMUs. Udhaifu huu unadhihirishwa kwa uwepo wa mialo isiyo rasmi.

Takwimu za uvuvi katika mialo hazikusanywi kwa sababu makampuni binafsi yaliyopewa kazi hiyo lengo lao ni ukusanyaji wa mapato pekee na si takwimu za uvuvi. Pia kuwepo kwa ushirikiano duni kati ya viongozi wa serikali ya kijiji na viongozi wa BMU na kukosekana kwa mafunzo ya msingi ya ukusanyaji wa takwimu kwa BMUs.

Wizara imeweka kipimo cha urefu wa sangara anayefaa kuvuliwa kuwa kati ya sentimita 50 and 85 ingawa hakuna kiwango cha juu cha kiasi cha sangara kuvuliwa kwa mwaka. Pia hakuna udhibiti wa kutosha wa uvuaji kumekuwa na udhibiti mdogo wa samaki wachanga.

6.3.3 Hatua dhidi ya Uvuvi haramu, usioripotiwa na kudhibitiwa

Ukaguzi umegundua kwamba, kumekuwa na ongezeko la matumizi ya zana haramu katika Ziwa Victoria. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 na 2011/2012 ongezeko ilikuwa kutoka 6415 hadi 146, 657 katika mikoa yote mitatu ya kanda ya ziwa. Ongezeko hili limechangiwa na kuongezeka kwa matumizi ya kokoro kwa asilimia 368 kutoka 394 kwa 145,302. Hii ni kwa sababu ya mahitaji makubwa ya samaki katika viwanda, jamii husika na ongezeko la soko la samaki wachanga nchi za jirani za Congo, Rwanda, Sudan Kusini na Burundi.

Wafanyabiashara haramu wa samaki hawafikishwi mahakama kwa kiwango cha kuridhisha hii inadhihirishwa kwa asilimia ndogo ya kesi zilizofunguliwa. Kituo cha Uvuvi doria katika mkoa wa Mwanza kesi nyingi hazikupelekwa mahakamani kwa sababu ya maafisa kutokuwa na ujuzi wasingi wa namna ya kufungua kesi pamoja na kuendesha mashtaka. Hata kwa zile kesi ambazo zilipelekwa mahakamani na kufunguliwa jalada, zilichukua muda mrefu kukamilika na gharama za uendeshaji kuwa kubwa. Hali hii inatokana na waendesha mashtaka kuchukua muda mrefu katika kufanya uchunguzi.

Uratibu wa taarifa za Uvuvi haramu, kutoripotiwa na kutodhibitiwa kwa Uvuvi

Wizara ya Mifugo na maendeleo ya Uvuvi “MLFD” ilikuwa na lengo la kuanzisha hifadhidata kwa ajili ya utoaji wa taarifa kwa wakati ifikapo Juni 2010. Hata hivyo, wizara haikuweza kutekeleza lengo hilo la kuanzisha mfumo wa kushirikiana taarifa hizo hali ambayo imesababisha ukusanyaji hafifu wa takwimu na taarifa za kiasi cha samaki wanaovuliwa, akiba iliyopo na taarifa za ki-intelligencia kutokomeza uvuvi haramu. Pia, hakuna muundo mzuri na unaofanyakazi katika mtiririko wa taarifa kati ya vikundi vya usimamizi wa mialo (BMUs) na halmashauri za wilaya na kati vituo vya uvuvi doria.

Kampeni za uelimishaji juu ya “Uvuvi haramu, kutoripotiwa na kutodhibitiwa”

Kampeni za uelimishaji dhidi uvuvi haramu, kutoripotiwa na kutodhibitiwa kwa shughuli uvuvi katika Ziwa Victoria hazikutekelezwa ingawa zilikuwa kwenye mipango. Mipango hiyo haikuonyesha itafanyika wapi na elimu hiyo kama itajikita katika maswala ya kudhibiti uvuvi haramu, usioripotiwa na kudhibitiwa.

6.4 Tulichohitimisha

6.4.1 Udhibiti wa uvuvi haramu haujatekelezwa vya kutosha

Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi haijachukua hatua za dharura kuokoa hali ya kushuka kwa kiasi cha sangara katika Ziwa Victoria. Idara haijaweka mipango ya kuzuia uvuvi wa wazi “open access” ili kudhibiti kushuka kwa kiasi cha sangara. Pia, taratibu za leseni katika wilaya hazifuatwi ipasavyo hivyo kuletelea wavuvi wengi na vyombo vya uvuvi kutosajiliwa na BMUs.

6.4.2 Jukumu la ufuatiliaji kuzuia kupungua kiwango cha Sangara Ziwa Victoria halikutekelezwa ipasavyo

Wizara ya maendeleo ya Mifugo na Uvuvi imetekeleza kwa kiasi kidogo viwango vya udhibiti vilivyopo ili kupunguza tatizo la uvuvi kupita kiasi. Vituo vya Uvuvi doria vimekuwa vikipokea kiasi cha

asilimia 1.3 hadi 10.3. ya maduhuli yaliyokusanywa vituoni ili kuendesha shughuli za doria katika vituo vyao, pia Halmashauri hazina mfumo wa mgao wa fedha kwa BMUs ambao umeathiri ukusanyaji wa takwimu za samaki wanaotua katika mialo na hivyo basi takwimu hizo hazikusanywi. Wizara nayo, haijachukua hatua za kutosha kusimamia kiasi cha sangara wanaovuliwa kwa mwaka kinadhibitiwa.

6.4.3 Jitihada kidogo zimechukuliwa dhidi ya Uvuvi haramu, usioripotiwa na kudhibitiwa

Imebainika kuwa kuna utekelezaji dhaifu wa sheria za uvuvi katika Halmashauri zote zilizotembelewa pamoja na vituo vya Usimamizi, udhibiti na doria Uvuvi (MCS), Kasi ya uvuvi haramu hailingani na kasi ya wavuvi haramu wanaokamatwa. Kituo cha Usimamizi, udhibiti na doria uvuvi (MCS) na wilaya kanda ya ziwa zinazojihusisha na uvuvi hazikuweka juhudi na kipaumbele katika kupambana na uvuvi haramu. Kuna matukio ambayo vyombo vya uvuvi vikijihusisha na uvuvi haramu lakini adhabu zinazotolewa ni kidogo kiasi cha kutoweza kuwa njia ya kutokomeza uvuvi haramu na kuwa fundisho kwa wavuvi haramu wengine.

6.5 Tulichopendekeza

6.5.1 Udhibiti Uvuvi wa sangara ili kunusuru kiasi cha sangara kinachokadiriwa kuwepo kisitoweke

Wizara ya maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ihakikishe kwamba:

1. Uingiaji katika shughuli za uvuvi ziwani unadhibitiwa kwa njia ya usajili na utoaji wa leseni kwa vyombo vya uvuvi na wavuvi.
2. Kuwe na namna ya kujua kiasi cha sangara waliovuliwa na mtawanyo wa vyombo na zana za uvuvi zinazoingia ziwani.
3. Inatekeleza swala la msimu wa kufunga shughuli za uvuvi ili kulinda maeneo ya mazalia na maeneo ya makuzi ya samaki
4. Ufugaji wa samaki unatiliwa mkazo ili kukidhi mahitaji

- yaliyopo
5. Kuwe na mgawanyo wa rasilimali ambao unazingatia vigezo vya ufanisi katika maswala ya kudhibiti uvuvi.
 6. Ushirikiano kati yake na TAMISEMI unaboreshwa
 7. Kuimarisha ushirikiano kati ya nchi wanachama katika kushughulikia tatizo la kupungua Sangara Ziwa Victoria.

TAMISEMI inapaswa kuhakikisha kwamba:

1. Serikali za mitaa (Halmashauri) zenye shughuli za uvuvi zinadhhibiti uingiaji katika shughuli za uvuvi kwa kuimarisha na kuzingatia usajili na kutoa leseni kwa vyombo vya uvuvi na wavuvi.
2. Serikali za mitaa (halmashauri) zinatunga sheria ndogo ndogo kuwezesha kutekeleza muundo imara wa kisheria katika kudhibiti uvuvi haramu katika maeneo yao.

6.5.2 Uratibu/Ufuatiliaji wa shughuli za Uvuvi katika Ziwa Victoria

Wizara ya maendeleo ya Mifugo na Uvuvi inapaswa kuhakikisha kwamba:

1. Utendaji wa sekta ya Uvuvi unaratibiwa na kutathminiwa ipasavyo
2. Utendaji wa shughuli za Usimamizi, Udhibiti na Doria Uvuvi (MCS), unaratibiwa na kutathminiwa ipasavyo
3. Njia za udhibiti zilizowekwa vinaratibiwa na kutathminiwa mara kwa mara
4. Kuna mfumo ambao utawasaidia vikundi vya usimamizi wa mialo (BMUs) kuwa na fedha za kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo.
5. Inajenga mahusiano ya kazi ya karibu na halmashauri zenye shughuli za uvuvi.

TAMISEMI inapaswa kuhakikisha kwamba:

1. Halmashauri zenye shughuli za uvuvi kanda ya ziwa zinaratibu na kufadhili shughuli za uvuvi za BMUs ipasavyo;

- na
2. Halmashauri zenye shughuli za uvuvi kanda ya ziwa zinaratibu na kutathmini njia za udhibiti wa shughuli za uvuvi mara kwa mara.

6.5.3 Hatua zinachukuliwa ili kupambana na Uvuvi haramu, usioripotiwa na kutodhibitiwa kwa Uvuvi.

Wizara ya maendeleo ya Mifugo na Uvuvi inapaswa kuhakikisha kwamba:

1. Inatekeleza Mpango kazi wa kanda wa nchi wanachama wa kutokomeza uvuvi haramu, usioripotiwa na kudhibitiwa kwa kuboresha shughuli za uratibu wa shughuli za uvuvi, udhibiti na doria;
2. Inaanzisha hifadhidata “database” na kufanya mapitio ya taarifa hizo mara kwa mara kwa ajili ya kubadilishana habari na Taasisi ya Uvuvi Ziwa Victoria “LVFO”, Vituo vya Usimamizi, Udhibiti na Doria Uvuvi, Halmashauri zenye shughuli za uvuvi kanda ya ziwa na wadau wengine.
3. Kampeni za uelimishaji kwa wadau wote wa Ziwa Victoria zinafanyika ipasavyo
4. Hatua muhimu za kisheria zinachukuliwa dhidi ya waharifu wote

TAMISEMI inapaswa kuhakikisha kwamba:

1. Halmashauri zinachukua hatua za kisheria dhidi ya waharifu wote.

SURA YA SABA

UDHAIFU ULIOGUNDULIWA WAKATI WA UKAGUZI KATIKA KAZI ZA SERIKALI

Kwa kuzingatia malengo na matokeo ya ukaguzi yaliyopatikana katika kaguzi tano zilizofanyika kama zinavyosomeka katika muhtasari wa taarifa hii ya majumuisho, Kuna maswala ambayo serikali inahitajika kuyashughulikia kuhakikisha kwamba inasimamia shughuli zake kwa tija na ufanisi.

7.1 Madhaifu ya Jumla yaliyoonekana katika maeneo yaliyokaguliwa.

Maswala ya madhaifu hayo ya jumla ni kama ifuatavyo:-

7.1.1 Usimamizi mdogo wa Ukaguzi

Ukaguzi wa shughuli za serikali ni mojawapo ya nyenzo za udhibiti na ufuatiliaji ambazo zinaweza kutoa uhakika juu ya hali halisi ya shughuli mbalimbali zinazotekelezwa kulingana na viwango vilivyowekwa ili kuleta mabadiliko chanya. Hata hivyo, uchambuzi wa audit tano ambao muhtasari wake upo katika sura ya 2 hadi ya 6 unaonyesha kuwa usimamizi mdogo wa ukaguzi wa shughuli za serikali ilionekana kuwa ni moja ya madhaifu/mapungufu ya jumla yaliyoonekana katika shughuli za serikali.

Kwa mfano, katika ukaguzi wa ufanisi wa ukaguzi wa usalama barabarani na ukomo wa mwendokasi, ukaguzi wa usalama barabarani ulibaini usimamizi hafifu. Kaguzi zilikuwa hazina mipango kuoyesha mwelekeo na kukosa miongozo ya kaguzi za usalama barabarani.

Vilevile, katika ukaguzi wa ufanisi wa usalama mahali pa kazi mapungufu yaliyojitokeza yanahusiana na ukaguzi ni mipango duni ya ukaguzi ya usalama mahali pa kazi “OHS”, maeneo ya kazi yaliyosajiliwa kutokaguliwa ipasavyo, utunzaji hafifu wa kumbukumbu za taarifa za ukaguzi na upungufu wa ufuatiliaji wa matokeo ya ukaguzi.

Kwa upande wa usimamizi wa miradi ya ujenzi katika Serikali za Mitaa, ukaguzi ni moja ya matatizo yaliyobainika hii inatokana na kutofanya kaguzi za moja kwa moja wa miradi inayotekelezwa ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa tija.

Ukaguzi usioridhisha unaofanyika na maafisa uvuvi wilaya pamoja na vituo vya Usimamizi, Udhhibiti na Doria Uvuvi (MCS), katika kudhubiti shinikizo la uvuvi wa sangara katika Ziwa Victoria ili kuhaakikisha wavuvi wanatumia zana zinazokubalika kisheria na kuvua samaki ambao wapo katika vipimo vilivyosahihi. Haya ni matatizo ya ukaguzi yaliyobainika katika ukaguzi wa usimamizi wa uvuvi katika Ziwa Victoria.

7.1.2 Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na tathmini ni moja ya udhaifu mkubwa uliobainika kwa ujumla katika kaguzi tano za ufanisi kama zinavyooneshwa katika muhtasari wa taarifa hii. Mapungufu ya ufuatiliaji na tathmini ya ukaguzi wa usalama barabarani yalibainishwa katika ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa usalama barabarani na ukomo wa mwendokasi. Mfumo wa Taifa kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini wa ajili ya shughuli za ukaguzi wa usalama barabarani bado haujatengenezwa.

Ukosefu wa mfumo bora wa kufuatilia na kutathmini shughuli za Usalama mahali pa kazi umebainika katika ukaguzi wa ufanisi wa usalama mahali pa kazi. Ufuatiliaji na tathmini dhaifu unaofanyika katika ngazi ya Taifa na taasisi husika katika ukaguzi wa ufanisi wa mfumo wa bajeti, Pia imebainika kuwa kuna udhaifu mkubwa katika usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo .

Pia, katika ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa uvuvi Ziwa Victoria, masuala yanayohusiana na ufuatiliaji na tathmini kama vile utendaji wa kisekta haujafuatiliwa na kutathminiwa vyakutosha. Utendaji wa shughuli za MCS haujafuatiliwa na kutathminiwa vya kwa kutosha, Vigezo vya udhibiti ni nadra kufuatiliwa na kutathminiwa na Utendaji wa BMUs hautathminiwi vya kutosha.

7.1.3 Mipango dhaifu

Udhaifu katika kupanga mipango ni moja ya maeneo yaliyobainika

katika kaguzi zote za ufanisi zilizofanyika. Kuna mipango isiyotosha ya ukaguzi wa usalama barabarani, kaguzi za ukomo wa mwendokasi na usalama barabarani hazina mipango madhubuti katika kutatua maeneo hatarishi ya usalama barabarani na alama za ukomo wa mwendokasi hazijapangwa kulingana na sera, kanuni na miongozo ya ukaguzi iliyopo. Pia mipango ya shughuli za usalama mahali pa kazi haina mipango madhubuti katika ngazi mbalimbali.

Vile vile katika ukaguzi wa ukaguzi wa usimamizi wa miradi ya maendeleo katika Serikali za Mitaa, mipango ya kazi za ujenzi wa miradi ya maendeleo haifanyiki kwa umakini ili kudhibiti ucheleweshaji wa kukamilika kwa miradi, ongezeko kubwa la gharama, na kazi zenye ubora usioridhisha; miradi iliyopungwa kutekelezwa kutokutengewa fedha za kutosha na hivyo kupelekea ucheleweshaji mkubwa wa kukamilisha miradi hiyo; mipango ya mwaka ya manunuzi inaandaliwa ila haifuatwi na hii ni kutokana na mipango hiyo kutokuwa halisia

Katika usimamizi wa shughuli za Uvuvi katika Ziwa Victoria imeonekana kuna ukosefu wa mipango ya kutathmini utendaji wa vituo vya usimamizi, udhibiti na doria- uvuvi “MCSs” na vikundi vya usimamizi wa mialo “BMUs” unaofanywa na Mizara na Serikali za Mitaa husika, Ulionekana kuwa ni moja ya matatizo ukijumuisha na ukosefu wa mipango kazi na mipango ya maendeleo.

7.1.4 . Uhaba katika Ugawaji wa Rasilimali

Mgawanyo wa rasilimali ni miongoni mwa matatizo makubwa yaliyobainishwa katika kaguzi zote tano za ufanisi zilizofanywa ambazo zinahitaji hatua kubwa kuchukuliwa ili kuboresha utendaji kazi. Imebainika kwamba kuna uhaba wa mgawanyo wa rasilimali kwa ajili ya kushughulikia wavunjaji wa sheria barabarani, ukaguzi uliofanywa katika maeneo ambayo hayahitajiki au ambayo yana matukio machache ya ajali za barabarani kwa upande wa OSHA haina mfumo wa wazi wa kupata rasilimali na mgawanyo wake.

Vilevile, katika ukaguzi wa usimamizi wa shughuli za uvuvi Ziwa Victoria, imebainika kuwa kuna uhaba wa fedha katika kishemu cha usimamizi, udhibiti na doria (MCS) kwa ajili ya kufanya kaaguzi mara kwa mara , ukosefu wa mfumo uliowazi wa fedha ili kuhakikisha uendelevu wa vikundi vya usimamizi wa mialo na pia kutojulikana kwa

uwiano ambao BMUs wanatakiwa kupata kutoka halmashauri husika.

7.1.5 Uratibu wa wadau ni mdogo/hauridhishi

Kwa mujibu wa uchambuzi wetu wa taarifa tano za kaguzi za ufanisi zilizofanyika, udhaifu katika kuratibu wadau muhimu ni swala lililojitokeza karibu katika ripoti zote tano. Kwa mfano, udhaifu kwa wadau katika kutoa taarifa za muhimu kwa ajili ya mapitio ya ukomo wa mwendokasi Tanzania swala hili limebainika katika ukaguzi wa ufanisi wa Usimamizi wa usalama barabarani na ukomo wa mwendokasi.

Maswala yanayohusiana na hayo yaliyobainika ni ukosefu wa uratibu kati ya OSHA na wadau wengine muhimu ambao wangeweza kutoa baadhi ya taarifa kama vile wadau hao ni TIC, BRELA, CRB, TRA and NBS; Uratibu hafifu kati ya wadau husika katika, kupanga, kutekeleza, ufuatiliaji wa miradi ya ujenzi na tathmini yake ili kuhakikisha ufanisi wake.

Sawasawa na ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa shughuli za uvuvi Ziwa Victoria, ilibainika kuwa kuna kuna uratibu usioridhisha katika kuratibu shughuli za uvuvi kati ya divisheni ya Uvuvi katika ngazi ya Taifa, vituo vya MCS katika ngazi ya mkoa na maasifa Uvuvi katika ngazi ya Serikali za Mitaa pamoja na Sekretariati ya mkoa inayoshughulikia maswala ya Uvuvi.

7.1.6 Utekelezaji duni wa adhabu

Katika kaguzi tano za ufanisi zilizofanyika, imefahamika kuwa matumizi ya adhabu kama vile faini na utekelezaji mwingine wa adhabu hakufanyika kwa kiasi cha kutosha. Katika ukaguzi wa usalama barabarani na ukomo wa mwendokasi, ilibainika kuwa adhabu kwa wavunja sheria za barabarani haina ufanisi katika kutokomeza uhalifu huo kwani dereva huyohuyo huwa anarudia makosa huku akijua adhabu zitolewazo hazina makali.

Katika ukaguzi wa ufanisi wa OHS imeonekana kuwa kuna udhaifu katika kutekeleza sheria kwa waajiri kuhusiana na usajili na utekelezaji wa mapendekezo ya OSHA. Vilevile Katika ukaguzi wa usimamizi wa miradi ya maendeleo katika Serikali za Mitaa ukosefu wa vikwazo/adhabu kwa wakandarasi wanaoshindwa kukamilisha kazi kwa muda au kufanya kazi zilizo chini ya kiwango.

Kadhalika, katika ukaguzi wa usimamizi wa shughuli za uvuvi masuala yafuatayo yalibainishwa; utoaji wa adhabu na utekelezaji wa sheria na kanuni za uvuvi zilizopo hazikutekelezwa ipasavyo katika kupunguza tatizo la uvuvi haramu, usioripotiwa na kudhibitiwa; udhaifu katika Serikali za Mitaa na vituo vya doria kwa kutosimamia vya kutosha kubaini na kutia mbaroni wavuvi haramu ukilinganisha na hali ya uhalifu ilivyo katika ziwa; pia kuna utekelezaji hafifu wa sheria na ufanyikaji wa doria hafifu katika maeneo ya mipakani na maeneo tete ya mazalia ya samaki.

7.1.7 Mfumo dhaifu wa usimamizi wa Taarifa “Data”

Hili pia ni miongoni mwa madhaifu ya jumla katika kaguzi tano zilizozungumziwa katika ripoti hii. Kuna ukosefu wa kuratibu hifadhidata “database” muhimu kwa ajili ya mapitio ya ukomo wa mwendokasi, Ukosefu wa historia ya data za waharifu wa barabarani, ukosefu wa data za kuaminika na data za kina za ajali za barabarani.

Aidha, ukosefu wa taarifa kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini shughuli za OHS, kutokuwa na data za kuaminika za kupata makisio ya mapato, ukosefu wa hifadhidata ya kuaminika kwa ajili ya utoaji wa taarifa za uvuvi kwa wakati. Hii imebainika katika ukaguzi wa uvuvi uliofanyika.

7.2 Hitimisho

Uchambuzi wa masuala jumla yaliyobainishwa katika kaguzi tano za ufanisi na kaguzi maalum zilizofanyika zinatungoza kuhitimisha kwamba baadhi ya malengo yaliyopangwa na serikali yanaweza kuwa vigumu kufikiwa kutokana na madhaifu mengi yaliyobainishwa wakati ukaguzi.

Madhaifu hayo ni katika mipango ya shughuli mbalimbali za serikali, kufanya kaguzi katika sekta husika, mgawanyo wa rasilimali, uratibu wa wadau muhimu katika sekta husika, utekelezaji wa adhabu mbalimbali na mfumo wa usimamizi wa data katika vyombo mbalimbali serikali huathiri kufikiwa kwa malengo ya kiuchumi, tija na kiufanisi “Economy, Efficiency and Effectiveness” katika programu, shughuli na miradi ya serikali

7.3 Mapendekezo kwa Ofisi ya Waziri Mkuu

7.3.1 Usimamizi wa kaguzi

Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe kwamba vyombo vya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa vinafanya yafuatayo kuhusiana na usimamizi wa kaguzi za program za serikali:-

1. Kaguzi za shughuli mbalimbali za Serikali inapangwa ipasavyo
2. kaguzi zinaelekezwa kwa namna ambayo zitatatua matatizo katika maeneo hatarishi katika sekta husika
3. Kaguzi zisimamiwe ipasavyo
4. Kuwe na miongozo rasmi kwa ajili ya kufanya kaguzi mbalimbali
5. Kuweka kumbukumbu za kutosha za Matokeo ya kaguzi
6. Kuna ufanisi katika ufuatiliaji wa matokeo ya kaguzi

7.3.2 Ufuatiliaji na tathmini

Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe kwamba vyombo vya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa vinafanya yafuatayo kuhusiana na Ufuatiliaji na tathmini ya progamu za serikali:-

1. Inafuatilia na kutathmini utendaji wa vyombo vyote vya serikali Tanzania
2. Vyombo vyote vya Serikali vinaandaa mipango ya ufuatiliaji na kutathmini M&E na kuitekeleza ipasavyo na kuhakikisha taarifa za utendaji zinaandaliwa kwa vipindi.
3. Vyombo vyote vya serikali vinaandaa viashiria muhimu vya utendaji na kuvipima ili kutathmini utendaji wao
4. Kutengeneza/kuandaa utaratibu Taifa wa kina wa ufuatiliaji na kutathmini shughuli/proramu katika ngazi ya Taifa.

7.3.3 Mipango ya Shughuli za Serikali

Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe kwamba vyombo vya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa vinafanya yafuatayo kuhusiana na Mipango ya shughuli za serikali:-

1. Kufanya tathmini ya mahitaji (juu ya rasilimali ili kutekeleza shughuli na programu) za Wizara, idara, wakala na Serikali za mitaa pale inapofanya mchakato wa kupanga mipango;
2. Taasisi na vyombo vyote vya serikali vinaandaa mipango ya kuendesha shughuli zao na mipango ya maendeleo;
3. Kuna mawasiliano ya kutosha na ya wakati katika Mipango ya maendeleo na mipango ya kawaida kwa vyombo vya serikali husika; na
4. Mipango ya matumizi ya vyombo vya serikali viendane na vipaumbele vya kissekta.

7.3.4 Mgawanyo wa Rasilimali

Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe kwamba vyombo vya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa vinafanya yafuatayo kuhusiana na mgawanyo wa rasilimali kuwezesha shughuli za serikali:

1. Kuna mfumo wa wazi wa kupata rasilimali na mgawanyo katika sekta na shughuli mbalimbali za serikali;
2. Mgawanyo wa rasilimali unafanyika kwa kuangalia vipaumbele na hatari zilizopo.

7.3.5 Uratibu kati ya Wadau Muhimu

Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe kwamba vyombo vya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa vinafanya yafuatayo kuhusiana na uratibu wa kati ya wadau muhimu katika kutekeleza programu za serikali.

1. Uratibu wa kifanisi kati ya taasisi/vyombo vya serikali na wadau mbalimbali wenye wajibu wa kutoa taarifa au huduma muhimu Tanzania. Kazi hii inabidi kuongozwa na Ofisi ya waziri Mkuu yenyewe; na
2. Kuna mfumo imara wa kuratibu kwa ajili ya kufuatilia kazi za idara, divisheni na visehemu katika ngazi ya taasisi ili kuhakikisha ufanisi wa kazi husika.

7.3.6 Utekelezaji wa sheria

Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe kwamba vyombo vya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa vinafanya yafuatayo kuhusiana na utekelezaji wa adhabu mbalimbali zinazotolewa kwa wahalifu katika kutekeleza programu za serikali.

1. Hatua sahihi za kisheria zinachukulia kwa taasisi za kiserikali/waharifu ili kuepuka hasara au utendaji mbovu
2. Hatua madhubuti za kisheria zinatekelezwa ipasavyo katika kupunguza vitendo haramu vya ukiukwaji wa sheria
3. Hatua za kisheria zinazochukuliwa zinawekwa wazi kwa umma ili kuleta mwamko kwa umma juu ya hatari ya kutofuata sheria husika

7.3.7 Mfumo wa Usimamizi wa data

Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe kwamba vyombo vya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa vinafanya yafuatayo kuhusiana na mfumo wa usimamizi wa data katika kutekeleza programu za serikali.

1. Kuna uratibu wa hifadhidata muhimu kwa ajili ya kupata taarifa kutoka katika taasisi mbalimbali za serikali.
2. Kuna data za kuaminika na za kina kwa ajili ya utoaji wa taarifa kwa shughuli na program za serikali
3. Kuna hifadhidata za kuaminika kwa ajili ya kutoa taarifa

Kiambatanisho 1: Muhtasari wa udhaifu katika uendeshaaji wa shughuli za Serikali ulioonekana katika ukaguzi wa ufanisi na maalumu

Udhaifu ulioonekana	Usimamizi wa ukaguzi Trafiki na mipaka ya kasi	Afa na Usalama Kazini	Usimamizi wa miradi ya maendeleo katika Serikali za Mitaa	Usimamizi wa shughuli za Uvuvi katika Ziwa Victoria	usimamizi wa manunuzi ya vifaa vya TEHAMA katika sekta ya Umma
<p>Upungufu katika usimamizi wa ukaguzi</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Usimamizi duni wa ukaguzi wa trafiki • wakaguzi wa trafiki kutopewa maelekezo sahihi • Ukosefu wa miongozi ya kufanyia ukaguzi wa trafiki 	<ul style="list-style-type: none"> • Upungufu katika mipango ya ukaguzi wa afa na usalama kazini • Maeneo ya kazi yaliyosajiliwa kutokaguliwa ipasavyo • Utunzaji mbovu wa taarifa ya ukaguzi • Kutokuwepo kwa ufuatiliaji wenye tija katika matokeo ya ukaguzi 	<ul style="list-style-type: none"> • Ukosefu wa ukaguzi wa miradi ya ujenzi iliyo chini ya Serikali za Mitaa • ili kuangalia utekelezaji wake na kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa tija. 	<ul style="list-style-type: none"> • Upungufu wa ukaguzi uliotakiwa kufanyika na 'DFOs' na vituo vya 'MCS' kudhibiti shimikizo la uvuvi wa sangara kuhakikisha kwamba wavuvi wanatumia vifaa sahihi vya kuvulia, wanavua aina na ukubwa sahihi wa samaki 	<ul style="list-style-type: none"> • Kamati za ukaguzi za taasisi hazifanyi kazi zao kikamilifu, kwani hawaandai taarifa ya ubora wa vifaa vilivyopokelewa
<p>Udhaifu katika Ufuatiliaji na Tathmini</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Upungufu wa ufuatiliaji na tathmini ya ukaguzi wa trafiki • Kutokuwepo kwa utaratibu wa taifa kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini shughuli za ukaguzi wa trafiki. 	<ul style="list-style-type: none"> • Ukosefu wa mfumo bora wa kufuatilia na kutathmini shughuli za afa na usalama kazini zilizofanyika 	<ul style="list-style-type: none"> • Ukosefu wa Ufuatiliaji na tathmini toshelezi za miradi ya maendeleo katika Serikali za Mitaa 	<ul style="list-style-type: none"> • Upungufu katika ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Sekta • Utendaji wa shughuli za 'MCS' haufuatiliwi na kutathminiwa ipasavyo. • Vyombo udhibiti ni nadra na 	<ul style="list-style-type: none"> • Taasisi za manunuzi kutotoa taarifa juu ya utendaji wa wauzaji katika kutekeleza mikataba. Kwa sababu hii baadhi ya wauzaji ambao hawakuweza kufanya vizuri katika baadhi

Udhaifu ulioonekana	Usimamizi wa ukaguzi Trafiki na mipaka ya kasi	Afya na Usalama Kazini	Usimamizi wa miradi ya maendeleo katika Serikali za Mitaa	Usimamizi wa shughuli za Uvuvi katika Ziwa Victoria	usimamizi wa manunuzi ya vifaa vya TEHAMA katika sekta ya Umma
Mipango duni	<ul style="list-style-type: none"> • Ukosefu wa mipango ya ukaguzi wa Trafiki • Mipaka ya kasi na ukaguzi na trafiki haipangwi kiusahihi kushughultikia maeneo hatari • Ishara za mipaka ya kasi hazijapangwa kiusahihi kulingana na sera zilizopo, maelekezo, kanuni na desturi bora 	<ul style="list-style-type: none"> • Upungufu katika mipango ya shughuli za afya na usalama kazini 	<ul style="list-style-type: none"> • Mipango ya kazi za ujenzi wa miradi ya maendeleo haifanyiki kwa umakini ili kudhibiti ucheleweshaji wa kukamitika kwa miradi, ongezeko kubwa la gharama, na kazi zenye ubora usioridhisha 	<ul style="list-style-type: none"> • kutathminiwa • Utendaji wa BMUs kutotathmini ipasavyo 	<ul style="list-style-type: none"> • Taasisi za manunuzi kutokuwa na mipango kwa ajili ya kufuatilia utendaji wa wauzaji kutoka awamu ya kuingia mkataba katika mchakato wa ununuzi na wakati wa awamu ya utekelezaji, nahawajaweza kutambua rasilimali zinazohitajika kwa
				<ul style="list-style-type: none"> • Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutokuwa na mipango kwa ajili ya kutathmini utendaji 'MCS' na 'BMUs' kwa mtiririko. • BMUs kutokuwa na mipango ya maendeleo na uendeshaji. 	<ul style="list-style-type: none"> • Pamoja na kuwa moja ya majukumu yao, PPD haijaweka vipaumbele vyao katika ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa manunuzi kwa miaka mitatu iliyopita.

Udhaifu ulioonekana	Usimamizi wa ukaguzi Trafiki na mipaka ya kasi	Afya na Usalama Kazini	Usimamizi wa miradi ya maendeleo katika Serikali za Mitaa	Usimamizi wa shughuli za Uvuvi katika Ziwa Victoria	usimamizi wa manunuzi ya vifaa vya TEHAMA katika sekta ya Umma
Upungufu katika mgawanyo wa rasilimali	<ul style="list-style-type: none"> Upungufu katika mgawanyo wa rasilimali kwa ajili ya wavunja sheria za trafiki Ukaguzi unafanyika katika maeneo ambayo yana uhitajaji mdogo 	<ul style="list-style-type: none"> Ukosefu wa mfano wa wazi kwa ajili ya kukusanya na kugawa rasilimali 	<ul style="list-style-type: none"> Miradi iliyopungwa kutekelezwa kutokutengewa fedha za kutosha na hivyo kupelekea ucheleweshaji mkubwa wa kukamilisha miradi hiyo Mipango ya mwaka ya manunuzi inaandaliwa ila haifuatwi na hii ni kutokana na mipango hiyo kutokuwa halisia 	<ul style="list-style-type: none"> Fedha zilizotolewa kwa udhibiti na idaraya ufuatiliaji zinatoa msaada duni katika ukaguzi wa mara kwa mara Ukosefu wa mfano wa wazi wa 	<ul style="list-style-type: none"> ajili ya ufuatiliaji wa wauzaji waliopo. PPD pia imeshindwa kuweka vipaumbele sahihi katika mipango yao kwa kuzingatia uzoefu wa vitendo. Kwa miaka mitatu mfululizo PPD imebadili matumizi 'misallocated' ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa mfumo wa ununuzi na kusababisha shughuli iliyodhamiriwa kutoanza.

Udhaifu ulioonekana		Usimamizi wa ukaguzi Trafiki na mipaka ya kasi	Afa na Usalama Kazini	Usimamizi wa miradi ya maendeleo katika Serikali za Mitaa	Usimamizi wa shughuli za Uvuvi katika Ziwa Victoria	usimamizi wa manunuzi ya vifaa vya TEHAMA katika sekta ya Umma
	au ambapo kuna matukio machache ya ajali za barabarani.	<ul style="list-style-type: none"> • Uratibu dhifu miongoni mwa wadau mbatimbali wanaowajibika kutoa taarifa muhimu kwa ajili ya marekebisho ya mipaka ya kasi katika Tanzania. 	<ul style="list-style-type: none"> • Ukosefu wa uratibu kati ya OSHA na wadau wengine muhimu ambao wangeweza kutoa baadhi ya taarifa kama vile TIC, CRB, TRA na NBS. 	<ul style="list-style-type: none"> • Uratibu usiyo na ufanisi miongoni mwa wadau katika upangaji na utekelezaji wa miradi ya ujenzi • Ukosefu wa mfumo imara wa uratibu kwa ajili ya kufuatilia uborawa kazi za wakandarasi wanaotekeleza miradi ya maendeleo 	<ul style="list-style-type: none"> • Upungufu wa utekelezaji wa jukumu la uratibu wa shughuli za uvuvi na: <ul style="list-style-type: none"> - DFD katika ngazi ya Taifa, - Vitengo vya 'MCS' vya mikoa katika ngazi ya kanda, na - DFOs katika ngazi ya Serikali za Mitaa 	

<p>Udhaifu ulioonekana</p> <p>Upungufu katika utekelezaji wa vikwazo/adhabu</p>	<p>Usimamizi wa ukaguzi Trafiki na mipaka ya kasi</p> <ul style="list-style-type: none"> Vikwazo/adhabu zisizokuwa na ufanisi kwa wavunja sheria za trafiki kwa madereva kurudia makosa kwa kuwa vikwazo/adhabu zinazotumika hazina ufanisi 	<p>Afyana Usalama Kazini</p> <ul style="list-style-type: none"> Udhaifu wa utekelezaji wa sheria ya waajiri kuhusu usajili na utekelezaji wa mapendekezo ya OSHA 	<p>Usimamizi wa miradi ya maendeleo katika Serikali za Mitaa</p> <ul style="list-style-type: none"> Ukosefu wa vikwazo/adhabu kwa wakandarasi wanaoashindwa kukamilisha kazi kwa muda au kufanya kazi zilizo chini ya kiwango 	<p>Usimamizi wa shughuli za Uvuvi katika Ziwa Victoria</p> <ul style="list-style-type: none"> vikwazo na adhabu zilizopo hazitekelezwi kiufanisi kupunguza uvuvi haramu, usiotolewa taarifa na usiodhibitiwa, dhaifu katika utekelezaji wa sheria katika Hatimashauri zote zilizotembelewa na vitengo vya 'MCS' ambapo wavuvi haramu hawakuwekwa mbaroni ikilinganishwa na uharamu walioufanya utekelezaji duni wa sheria na ufuatiliaji katika mpaka na maeneo tete 	<p>usimamizi wa manunuzi ya vifaa vya TEHAMA katika sekta ya Umma</p> <p>Taasisi ya manunuzi kutozingatia mikataba wakati wa kusimamia upokeaji wa bidhaa, vifungu vinavyohusu makato ya ucheleweshaji wa kukamilisha kazi 'liquidated damages' havitumiki kwa bidhaa zilizocheleweshwa.</p>
<p>Mfumo dhaifu wa usimamizi wa data</p>	<ul style="list-style-type: none"> Ukosefu wa hifadhidata ulioratibiwa muhimu kwa ajili ya mapitio ya mipaka ya kasi Ukosefu wa historia ya data ya wavunja sheria ya trafiki Ukosefu wa data ya kuaminika na ya kina juu ya matukio ya ajali za barabarani 	<p>Ukosefu wa taarifa kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini shughuli za afya na usalama kazini</p>	<p>Data zisizokuwa na uhakika kutumika kukadiriia gharama na muda wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi</p>	<p>ukosefu wa hifadhidata kwa ajili ya utoaji wa taarifa za uvuvi kwa wakati na sahihi</p>	

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA



National Audit Office

Our ethical values

The National Audit Office - Tanzania, being a Supreme Audit Institution, is a member of International Organization of Supreme Audit Institutions (INTOSAI)

We have a code of ethics which guides our daily audit work. In addition, employees are obliged to observe the Tanzania Public Service code of ethics and conduct and their respective professional codes of ethics.



OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI



Head Office

The controller and Auditor General, National Audit Office,
Audit House, Samora Avenue / Ohio Street
P.O.Box 9080, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 22 2115157 / 8, Fax: +255 22 2117527
Email: ocaq@nao.go.tz, Website:www.nao.go.tz

REGIONAL OFFICES (RESIDENT /AUDITORS)

ARUSHA
P.O.BOX 202 ARUSHA
027-2502453

DODOMA
P.O.BOX 950 DODOMA
023-2621759

KIGOMA
P.O.BOX 213 KIGOMA
028-2802807

MANYARA
P.O.BOX 391 BABATI
027-2530298

IRINGA
P.O.BOX 94 IRINGA
026-2702692

MBEYA
P.O.BOX 333 MBEYA
025 - 2502142

SHINYANGA
P.O.BOX 219 SHINYANGA
028-2762480

RUVUMA
P.O.BOX 245 SONGEA
025-26002340

RUKWA
P.O.BOX 169 SUMBAWANGA
025-0802282

SINGIDA
P.O.BOX 122 SINGIDA
026-2502246

MOROGORO
P.O.BOX 738
MOROGORO
023-2603004

TABORA
P.O.BOX 22 TABORA
026-2512447

KAGERA
P.O.BOX 719 BUKOBA
028-2220483

KILIMANJARO
P.O.BOX 646 MOSHI
027-27522625

MWANZA
P.O.BOX174 MWANZA
028-2500933

LINDI
P.O.BOX 24 LINDI
023-2202465

MTWARA
P.O.BOX 130 MTWARA
023-2333005

MUSOMA
P.O.BOX 423 MUSOMA
028-2622354

TANGA AUDIT BRANCH
P.O.BOX 113 TANGA
027-2646369

PWANI
P.O.BOX 30080 KIBAHA
023-2402032